# UCHUNGUZI WA TABIA ZA TONI KATIKA NOMINO ZA KIROMBO

*Mramba Peter, T (PhD)*
***Chuo Kikuu cha Mt. Augustino Tanzania***

***Ndaki Shiriki Jordan Morogoro***

***Idara ya Lugha***

***Baruapepe: mrambadoctor@gmail.com***

***Simu: +255763 090 215/ 785678465***

## IKISIRI

*Makala haya yanahusu uchanganuzi wa tabia za toni katika Nomino za Kirombo. Lengo kuu la makala haya ni kuchunguza tabia za ujitokezaji wa toni katika nomino za Kirombo na kanuni zinazotawala utokeaji huo. Aidha, malengo mahususi: kubainisha silabi inayohusishwa na Tonijuu Msingi (kuanzia sasa TJM) na mbili, kujadili tabia za utokeaji wa toni katika nomino za Kirombo na kanuni zinazotawala hutokeaji huo. Data ya Makala haya imetokana na utafiti mpana uliofanywa juu ya toni katika lugha ya Kirombo wilayani Rombo (2024) ambao uliongozwa na Nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru kwa kutumia Mkabala wa Tonijuu Msingi kama ulivyoasisiwa na Goldsmith (1976) na kuboreshwa na wanazuoni mbalimbali katika taaluma ya tonolojia. Aidha, mbinu za ukusanyaji data zilizotumika ni pamoja na mahojiano na ushuhudiaji. Katika mahojiano nomino ziliandaliwa kwa Kiswahili na watoataarifa walihitajika kuzitamka kwa Kirombo huku mtafiti akirekodi na kualamisha toni katika nomino hizo. Aidha, katika mbinu ya ushuhudiaji mtafiti alishuhudia kwa kushiriki. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuna tabia mbalimbali za kitoni zinazoleteleza utokeaji wa kanuni za kitoni ambazo hutofautiana kutegemeana na idadi ya silabi. TJM hupachikwa katika silabi ya kwanza ya shina la nomino. Kwa nomino za silabi mbili hadi ama tano au sita za shina hutawaliwa na kanuni ya udondoshaji, msambao wa tonijuu kuelekea kulia mwa shina, na uhamaji wa TJM kutoka silabi ya kwanza, zimetekelezwa baada ya utekelezwaji wa kanuni ya jumla ya Upachikaji wa TJM, katika uibuzi wa ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani. Aidha, ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika nomino za idadi ya silabi mbili hadi sita zote huanza na toni C katika KA ikifuatiwa ama na toni J au toni C katika silabi ya kwanza ya shina. Toni J hiyo usambaa hadi silabi ya mwisho kasoro mbili au moja kutoka mwishoni mwa shina la nomino husika.*

### Istilahi Muhimu

**Nomino:** *Neno linalotaja kitu,kiumbe, hali, dhana au tendo (Massamba, 2012; Saluhaya,2016).*
**Toni:** *Kipambasauti chenye uamilifu wa kileksika na kisarufi kinachoweza kupambanua maana za maneno na kuwakilisha njeo (Odden, 2005; Massamba, 2011: 171; Batibo, 2012).*

## 1.0 Utangulizi

Lugha ni mkusanyiko wa maneno yanayoundwa kwa sauti za nasibu. Sauti za lugha za binadamu ulimwenguni zina sifa ya kuwa na vipambasauti (Massamba, 2011). Vipambasauti ni vipengee vya uchanganuzi arudhi vinavyoweza kuandamishwa kwenye matamshi ya vitamkwa mbalimbali. Vipengee hivi ni pamoja na toni, mkazo, usilabi, kidatu, unazali, unguvunguvu, na nguvumsikiko. Makala haya yanahusika na kipengee cha toni ambacho ni kipambasauti chenye uamilifu wa kileksika na kisarufi kinachoweza kupambanua maana za maneno na kuwakilisha njeo (Odden, 2005; Massamba, 2011: 171; Batibo, 2012). Kwa mujibu wa wataalamu Heine na Nurse (2000), Nurse na Philipson (2003) na Batibo (2012), lugha nyingi za Kiafrika zina toni, ukiondoa zile za kundi la lugha za Kihamitiki kama vile Kishemu/Kihamu. Toni ni miongoni mwa sifa za kiarudhi[1] zilizowahamasisha wanaisimu kuchunguza vipengele mbalimbali vya lugha za Kibantu kwa kutumia Nadharia za taaluma ya fonolojia (Hyman, 2008). Suala la uwakilishi wa toni katika lugha lilishamiri zaidi hasa pale mwanaisimu Goldsmith (1976) alipoonesha mwanga wa uchanganuzi wa toni katika lugha mahususi kwa kutumia Nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru kama maboresho ya Nadharia ya Fonolojia Zalishi (Hayman, 2003: 4-6 na Massamba, 2011: 178).

[1] Arudhi ni sifa inayohusu mabadiliko ya vipambasauti kama vile kidatu, nguvumsikiko, tempo na lahani (Massamba, 2012).

## 2.0 Lugha ya Kirombo

Kirombo ni miongoni mwa jamiilugha za Kichaga. Kichaga hakina lugha moja inayoweza kuunganisha jamii ya Wachaga wote. Kila eneo (tarafa) lina kijilugha chake na kila kata ndani ya tarafa ina matamshi yake (Mramba, 2015). Kwa mujibu wa MLUTA (2009), jamii ya Wachaga ina jumla ya lugha asilia sita zinazotumika kwa mawasiliano ndani na nje ya eneo kitovu (Kilimanjaro). Lugha hizo ni *Kirombo, Kimachame, Kikahe, Kihusa, Kimochi na Kisia.* Hata hivyo, kuna lahaja zinazozungumzwa ndani ya jamii ya Wachaga kama vile Kiuru, Kiwoso, Kivunjo, Kichasu, Kimarangu na Kihanjo.

Kutokana na tafiti zilizofanywa na wataalamu mbalimbali kama Raum (1964), Polomé (1971), Van Spaandock (1971), Nurse na Philipson (1977), Heine na Nurse (2003), Martinet (2005), McHugh (2006), na Nelson (2013 na 2022), katika lugha za Kichaga kama vile Kiold Mochi, Kimachame, Kivunjo, Kikahe na Kisiha, wamebaini kuwa lugha hizo zina toni. Aidha, wamebaini mabadiliko ya utokeaji wa tabia za toni katika lugha hizo hayapo sawa jambo linalofanya baadhi ya lugha kuwa na zaidi ya 66% ya tonichini na chini ya 34% ya tonijuu katika maneno yake. Kulingana na matokeo ya tafiti hizo na ikizingatiwa kwamba Kirombo ni miongoni mwa jamiilugha za Kichaga, Kirombo pia kina toni ingawa haikuelezwa tabia yake ya utokeaji ikoje husussani kwa nomino.

Hii inatokana na ukweli kwamba lugha nyingi za Kibantu zina toni hususani zile za kundi la Naija-Kongo ambapo Kirombo hupatikana humo (taz. Nurse na Philipson, 2003). Batibo (2012) akimnukuu Van Spaandock (1971), anasema, kiasili jamiilugha za Kichaga zina toni, ambapo katika kila silabi na kila neno huwa na toni maalumu. Kutokana na maelezo hayo tunajiuliza: je, TJM nomino za Kirombo huhusishwa na silabi ipi? Je, tabia za toni katika nomino za silabi mbili hadi ama tano au sita za shina katika Kirombo zikoje na hutawaliwa na kanuni zipi? Maswali haya na mengine mengi tuliyokuwa tukijiuliza, yamejibiwa vyema katika sehemu ya 5.0 ambapo tabia za ujitokezaji wa toni katika silabi za nomino za silabi mbili hadi tano zimechanganuliwa.

## 3.0 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti wa Makala haya umeongozwa na nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru. Nadharia hii imeasisiwa na Goldsmith (1976). Wazo kuu la nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru (Kuanzia sasa FVH) ni kuwa, vipengee vyote vya kifonolojia, kikiwemo kipambasauti toni havina budi kuchukuliwa kuwa viko huru katika usemaji wa lugha yoyote iwayo. Vipengee hivyo vinapaswa kuchukuliwa katika upekee wake wa kujitegemea na kuwakilishwa kama vitu vilivyo huru lakini vinavyohusiana.

Katika kufanikisha hilo vipengee vyote huwakilishwa kwa kutumia rusu, yaani rusu ya vipandesauti, rusu ya kiimbotoni, rusu ya toni, na kadhalika. Rusu hizo huhusishwa kwa mistari ya uhusiano ambayo hudhibitiwa na Sharti la Ukubalifu linalodai kwamba, kila irabu ihusishwe na angalau toni moja, kila toni ihusishwe na angalau irabu moja, na mistari ya uhusiano isikingamane. Ukiukwaji wa sharti la ukubalifu huleteleza maumbo yasiyokubalika katika lugha husika. Nadharia ya FVH ina mikabala miwili ya uchanganuzi wa kipambasauti toni ambayo ni; mkabala wa uchanganuzi wa kiinitoni ambao huchombeza toni juu na mkabala wa Tonijuu Msingi kama msingi wa uchanganuzi wa toni. Katika Makala haya mkabala wa Tonijuu Msingi ndio uliotumika.

Mkabala wa Tonijuu Msingi (JM) hutumia toni juu (J) kama msingi wa uchanganuzi wa toni. Toni J huwekwa ama chini au juu ya irabu inamojitokeza. Mkabala huu ni matokeo ya kuboreshwa kwa mkabala wa Kiinitoni kama msingi wa uchanganuzi wa toni uliasisiwa na Goldsmith (1976), na kutumiwa na wataalamu wa isimu kama Massamba (1984), Ismail (2011, na 2016), na Mashauri (2012). Mkabala wa JM unazingatia uchanganuzi wa toni kwa kutumia Tonijuu Msingi (JM) katika kupata umbo la nje linalokubalika na wasemaji wazawa wa lugha. Vipengee vyote huwakilishwa kwa kutumia rusu zinazohusishwa kwa mistari ya uhusiano ambayo hudhibitiwa na Sharti la Ukubalifu kama ilivyo kwa mkabala wa uchanganuzi wa kiiinitoni kinachochombeza toni (KT). Miongoni mwa wanaisimu wanaotumia mkabala wa JM ni pamoja na Marlo (2007), Batibo (1990), Odden (1989), Ismail (2016), Hyman na Byarushengo (1984), Mramba (2020), kwa kutaja tu wachache. Mkabala wa JM umeteuliwa kukokotoa tabia za utokeaji wa toni katika nomino za silabi mbili hadi tano za shina kwa sababu uchanganuzi wake huleta uwazi zaidi katika ujitokezaji wa umbo la nje, upunguza idadi ya rusu katika ukokotozi wa umbo la nje kutoka umbo la ndani, ukilinganisha na mkabala wa Kiinitoni katika uchanganuzi wa toni kwa kutumia kiinitoni kinachochombeza toni juu.

## 4.0 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti ni njia ambazo hutumiwa na mtafiti katika kukusanya na kuchakata data. Mbinu hizi humwezesha mtafiti kupata data sahihi za utafiti, kuchagua mkabala, sampuli na vifaa ambavyo atatumia katika utafiti wake (Kothari, 2010). Aidha, mbinu za utafiti ni hatua au njia za makusudi zifanywazo na mtafiti ili kukwepa kujidanganya au kuwadanganya wengine watakaosoma ripoti yake. Mbinu zilizotumika ni pamoja na mahojiano na ushuhudiaji. Katika mahojiano nomino za silabi mbili hadi tano za shina ziliandaliwa kwa Kiswahili na

watoataarifa walihitajika kuzitamka kwa Kirombo huku mtafiti akirekodi na kualamisha toni katika nomino hizo. Aidha, katika mbinu ya ushuhudiaji Mtafiti alitembelea vijiwe viwili vya karata, ambapo wazee hupatikana majira ya jioni baada ya shughuli zao za kutwa. Mtafiti alishuhudia kwa kushiriki. Yaani, alishiriki kucheza karata kama sehemu ya timu au kundi pinzani. Kwa kufanya hivyo, ilikuwa rahisi kupata data sahihi ya matamshi kwa sababu watoa taarifa walikuwa huru kuzungumza wao kwa wao bila kujiandaa kutamka nomino fulani.

Data iliyokusudiwa katika utafiti huu ni nomino za silabi mbili hadi tano za shina za Kirombo katika kudhihirisha tabia za ujitokezaji wa toni ambazo zilipatikana baada ya mtafiti kuchambua taarifa zilizotolewa na watoataarifa kwa njia ya mahojiano na ushuhudiaji kutoka uwandani. Mbinu mwafaka za uteuzi wa maneno zilizingatiwa kama msingi wa kupata matokeo jumuifu, sahihi na kubalifu. Moja ya mbinu hizo ni kugawa nomino katika makundi kulingana na idadi ya silabi. Yaani, kuanzia muundo wa silabi mbili hadi tano za shina na pia, uasilia wa maneno husika (nomino za mkopo hazijatumika). Mbinu za utafiti zilihusisha mahojiano na ushuhudiaji kulingana na aina ya utafiti uliofanyika.

## 5.0 Ujitokezaji wa Tabia za Toni katika Nomino za Kirombo

Sehemu hii inahusu uwasilishaji na uchanganuzi wa data ya nomino na kanuni zinazotawala uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za Kirombo. Katika kutekeleza hilo, uchanganuzi wa data ya nomino tulioufanya umezingatia muundo wa nomino kulingana na idadi ya silabi. Hivyo, tumeanza kuwasilisha na kuchanganua data ya utafiti kwa kuanza na tabia ya nomino zenye muundo wa silabi chache kwenda zile zenye idadi nyingi ya silabi ambazo muundo wake ni mrefu zaidi. Aidha, sehemu ya mwisho ni hitimisho la sehemu hii kwa ujumla.

Katika sehemu hii tumeangazia tabia za toni katika nomino mbalimbali za Kirombo. Kulingana na data ya utafiti, nomino za Kirombo zipo katika makundi matatu kimuundo: moja ni kundi la nomino zenye kiambishi awali (KA) pekee. Kwa mfano: a) **i**défe ‘*debe’*, b) **i**kósha ‘*jani la mkomba’*, na c) **u**rísi ‘*uzi’*. Katika mfano huu, kiambishi /i-/ na /u-/ vilivyokozwa wino ni viambishi awali vya nomino za Kirombo. Nomino zote zina muundo ulioanza na kiambishi kisha shina la nomino.

Aidha, kundi la pili la nomino za Kirombo linahusu nomino zenye Kiambishi Awali Kitangulizi (KAK) na Kiambishi Awali (KA) kwa Pamoja. Kwa mfano, a) **i k** mú rya ‘*Kijinga cha moto kikubwa’* b) **i k** lyí ko ‘*kijiko kikubwa’* na c) **i k** bó bó ryi ‘*panyabuku mkubwa’*. Katika mfano huu mofimu zinazowakilisha KAK ni {i-} na {ka-} na mofimu zinazowakilisha KA ni {-k-}, na {-mu-}. Viambishi vya nomino za kundi la pili hufanya kazi mbalimbali ambazo huathiri nomino kwa kuzifanya zijibebeshe sifa inayozirejelea ndani yake. Yaani, sifa ya nomino hubebwa ndani ya nomino yenyewe na siyo kwamba hutengwa tofauti kama ilivyozoeleka kuwa unaweza kutanguliza nomino kisha sifa yake kwa mfano; **kijiko kikubwa,** ikiwa na maana kuwa sifa inayoelezea hali ya nomino **kijiko** ni kivumishi **kikubwa**. Kwa kundi hili la nomino za kirombo inaonekana sifa ya nomino hubebwa na kiambishi ambacho kipo ndani ya nomino yenyewe. Kiambishi awali kitangulizi {i-} cha nomino za Kirombo hufanya kazi ya kukubwasha nomino. Hii ina maana kwamba kiambishi kitangulizi /i-/ kikiondolewa katika nomino hizo sifa ya nomino hizo nayo huondoka. Kwa mfano nomino _kmúrya ‘*kijinga*’, _klyíko ‘*kijiko*’, _kbóbóryi ‘*panyabuku*’ na _muéngére ‘*mti wa majani ya mbuzi’*. Sifa zilizokuwepo katika nomino hizo kabla ya kuondolewa kwa kiambishi awali kitangulizi {i-} zimetoweka baada ya kuondoa kiambishi awali kitangulizi {i-}. Pia, kiambishi awali kitangulizi {ka-}katika mfano huo hufanya kazi ya udogoshi katika nomino za Kirombo kama inavyoonekana katika nomino **ka k** pá mbá sa ‘*ukuta mdogo’*. Pia, kiambishi awali kitangulizi {ka-} kikiondolewa katika muktadha wa nomino **ka k** pá mbá sa, nomino hii huwa _k pa mba sa ‘*ukuta*’. Mofimu {-k- na -mu-} katika nomino za kundi la pili hufanya kazi ya kuwa viambishi awali kutegemeana na aina ya nomino na mofimu hizi zikiondolewa katika muktadha wa nomino hufanya nomino hizo kupoteza maana au kutoeleweka kuwa zinarejelea nini hasa katika jamii lugha husika. Katika Kirombo, mofimu za KAK na KA zote hubeba toni C.

Kundi la tatu la nomino za Kirombo huwakisha nomino ambazo hazina KAK wala KA ukilinganisha na makundi mawili ya nomino tuliyoyaeleza hapo juu. Hivyo, katika kundi hili silabi ya kwanza ya shina ndiyo hujitokeza mwanzoni mwa nomino na huwa na toni C. Kwa mfano, a) sho ryó ko ‘*choroko’* b) mi mí na ‘*nyumba ya suti ya tope’* na c) na á nwa ‘*ua la mgomba’*. Katika Kirombo aina za nomino katika kundi la tatu ni chache sana ukilinganisha na idaidi ya nomino za kundi la kwanza na la pili. Pia, idadi ya ujitokezaji wa toni katika nomino za kundi hili hutegemea idadi ya silabi za shina.


Makundi hayo matatu ya nomino za Kirombo hutofautiana na tofauti zake husababishwa na viambishi. Yaani, kuna nomino zenye kiambishi awali pekee, nomino zenye viambishi awali na viambishi awali vitangulizi kwa pamoja wakati nomino nyingine hazina kiambishi awali wala kiamshishi awali kitangulizi. Pia, tumeona kuwa, idadi ya ujitokezaji wa toni katika makundi hayo hutegemea idadi ya silabi katika nomino husika na siyo kundi la

nomino. Hivyo, kutokana na sababu hiyo, uchanganuzi wa tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino za Kirombo utazingatia idadi ya silabi kwa kuanza na nomino zenye idadi cahche ya silabi kwenda zile zenye silabi nyingi za shina.

Baada ya kuona makundi matatu ya nomino za Kirombo kimofolojia, tunajiuliza Kiimbotoni Msingi cha nomino za Kirombo ni kipi? Tonijuu Msingi huhusishwa na silabi ipi katika shina la nomino za Kirombo? Katika makala haya **Kiimbotoni Msingi (KTM)** ni mzunguko mmoja wa kiimbotoni katika kupanda na kushuka kwa usemaji wa lugha zenye toni (§. Massamba 2011:173-174). Kulingana na majaribio anuwai yaliyofanywa, mtafiti amebaini kuwa Kiimbotoni msingi (KTM) cha nomino za Kirombo ni CJC. Aidha, mtafiti amebaini kuwa Tonijuu (TJM) inayojitokeza katika KTM kwenye nomino za Kirombo huhusishwa na silabi ya kwanza ya shina la nomino husika.

Hatahivyo, kutokana na matokeo ya kigezo cha kiisimu kilichotumika katika kubainisha silabi maalumu inayohusishwa na TJM katika nomino za Kirombo, tunaweza kuhitimisha kuwa, TJM inapaswa ipachikwe katika silabi ya kwanza ya shina la nomino za Kirombo. Kwa hiyo, matokeo ya kiisimu ya upachika wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina la nomino yanakinzana na yale ya kihistoria yanayoelezwa na Guthrie, (1971) na kushadidiwa na Matondo, (2003) kuwa, silabi yoyote katika shina la nomino inaweza kupachikwa TJM, kwa madai kwamba toni za nomino za mkopo katika lugha za Kibantu hazitabiriki. Matokeo ya kigezo cha kiisimu yamekinzana pia na madai hayo ya kihistoria kwa kuwa nomino zilizoshughulikiwa katika makala haya ni zile nomino za asili ya Kirombo tu bila kuhusisha nomino za mkopo kutoka lugha za kigeni ambazo ndizo Guthrie, (1971) alizotolea hitimisho kwa kigezo cha kihistoria. Kutokana na maelezo hayo, tunaweza kuunda kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM kwenye nomino za Kirombo kama ifuatavyo: (ambapo; KAK = Kiambishi Awali Kitangulizi, KA = Kiambishi Awali na SH = shina.

**Kanuni ya 1: Upachikaji wa Tonijuu Msingi katika Nomino za Kirombo**




Kanuni (1) inaeleza kuwa, tonijuu msingi (TJM) imehusishwe na silabi ya kwanza ya shina katika nomino za Kirombo. Hivyo, kanuni inasomeka kuwa, nomino inaweza kuwa na kiambishi awali kitangulizi (KAK) ambacho hufuatiwa na kiambishi awali (KA) na kuishia na shina la nomino ambapo, TJM huhusishwa na silabi ya kwanza ya shina linalohusika. Tufafanue kidogo hasa tunaposema 'nomino inaweza kuwa', hii ni kutokana na ukweli kwamba, katika Kirombo, siyo kwamba nomino zote zina KAK, bali nomino nyingi huanza kwa KA (ambacho ni irabu /i-/ au /u-/ katika umoja na mofimu {ma-} katika wingi wa nomino husika).

Kabla ya kufanya uchanganuzi wa tabia za toni katika nomino, ni vema tukaeleza kwamba, katika Kirombo KAK huoneshwa kwa kutumia kiambishi awali kitangulizi [-i-]. Aidha, ni vema ikafahamika kuwa muundo wa nomino za Kirombo huweza kuanza ama kwa Kiambishi awali kitangulizi [- i-] na kufuatiwa na kiambishi awali [-m/mu-na k,] au nomino za Kirombo zinaweza zikaanza kwa kiambishi awali (KA) pekee pasi kutanguliwa na KAK. Aghalabu viambishi hivi vimeonekana kuwa na toni C hasa vinapoangaziwa katika muktadha wa kitoni.

Katika sehemu hii tumechunguza jinsi tabia za toni zinavyojitokeza katika nomino za Kirombo. Katika kufanikisha hilo, tumechunguza nomino kwa kuzingatia idadi ya silabi katika nomino husika. Yaani, kwa kuanza na nomino zenye muundo wa silabi chache hadi zile nomino zenye idadi ya silabi nyingi za shina kama ifautavyo;

### 5.1 Ujitokezaji wa Tabia za Toni katika Nomino za Silabi Mbili za Shina

Kutokana na data ya utafiti, tumebaini kuwa tabia za ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi mbili za shina zipo katika makundi mawili: kundi la kwanza ni lile ambalo nomino zake zina KA ambapo tabia yake ya ujitokezaji wa toni ni CJC, wakati kundi la pili, nomino zake zina KA na KAK kwa pamoja na hivyo, kufanya tabia ya ujitokezaji wa toni katika kundi hili kuwa CCJC. Tuanze kuchanganua kwa kuchunguza data ya kundi la kwanza katika 1(a) hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| 1(a). | a) i dé fe | 'debe' |
| | b) i kó sha | 'jani la mkomba' |
| | c) i kú mbi | 'kienge' |
| | d) i kú nya | 'gunia' |
| | e) i sá ka | 'pori' |
| | f) i bí ba | 'pipa' |

Tukichunguza kwa umakini katika 1(a) tunaweza kubainisha masuala yafuatayo kimofolojia: data 1(a) ina nomino zenye silabi mbili za shina zenye maumbo tofautitofauti. Katika nomino za 1(b na c) silabi zake za mwisho zina muundo wa KKI na katika 1(d) silabi ya mwisho ina muundo wa KyI ambapo kiyeyusho kilichopo hakijatokana na mchakato wa uyeyushaji bali ni asili ya nomino hiyo katika Kirombo. Hivyo, ni hali ya kawaida kukuta silabi ya nomino yenye konsonanti zaidi ya moja. Nomino za silabi mbili katika 1(a) zina kiambishi awali kimoja ambacho ni /i-/. Pia, kiambishi awali /i-/ hufanya kazi kama kiambishi awali cha nomino katika hali ya umoja.

1(b)
- a) u ri si 'uzi'
- b) utufa 'unyayo'
- c) ulumi 'ulimi'
- d) uforyi 'mtego wa panya'
- e) ukofi 'kiganja'

Tukichunguza kwa umakini data 1(b) hapo juu tunaweza kubainisha mambo yafuatayo: Nomino zote zina idadi sawa ya silabi za shina ambazo ni mbili na zote zina mfuatano wa kimuundo unaoshabihiana isipokuwa silabi ya mwisho ya nomino uforyi katika 1(d) ambayo ina muundo wa KyI ambapo kiyeyusho [j] hakijatokana na mchakato wa uyeyushaji bali ni asili ya nomino yenyewe katika Kirombo. nomino zote zimeanza kwa kiambishi awali kimoja /u-/ ambacho pia ni kiambishi awali cha nomino za 1(b) katika umoja.

Tukichunguza kwa umakini katika data 1(a) na 1(b) hapo juu, tunaweza kugundua masuala ya kitoni kama ifuatavyo: katika data za makundi hayo mawili kuna toni J moja ambayo imejitokeza katika kila silabi ya kwanza ya shina. Pia, katika makundi hayo kuna toni C mbili ambazo moja hubebwa katika viambishi awali /i-/ na /u-/ na toni C ya pili imebebwa katika silabi ya mwisho ya shina. Ujitokeza huu wa toni ndio unaoleteleza tabia ya toni ya CJC katika kundi la kwanza la nomino za silabi mbili za shina.

Aidha, kanuni ya 1 ya upachikaji wa TJM iliyoundwa hapo juu, imetumika katika ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za 1(a) na 1(b). Kanuni ya 1 inaeleza kuwa, tonijuu msingi (TJM) inapaswa ipachikwe katika silabi ya kwanza ya shina la nomino za Kirombo wakati wa ukokotozi. Kwa kuzingatia kanuni hiyo, ukokotozi wa uibuzi wa tabia ya toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani ulianza kwa kupachika TJM kwenye silabi ya kwanza ya shina, kama inavyoonekana katika (1a) hapa chini:

i dé fe 'debe'
/i de fe/ 'Umbo la ndani'

J
|
1a. i de fe 'Upachikaji wa TJM'

C J C
| | |
i de fe 'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa'

[ i dé fe] 'Umbo la nje'

Tukichunguza kwa umakini ukokotozi wa nomino (1) hapo juu, tunagundua kwamba umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [*i dé fe*]. Matokeo ya ukokotozi (1) yanaonesha kuwa, tabia ya ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino [ i dé fe], huanza kwa toni C katika kiambishi awali /i-/, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina kisha kufuatiwa na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Aidha, ukichunguza kwa umakini ukokotozi wa (1) utagundua kwamba, kanuni ya 1 ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina la nomino imetekelezwa katika hatua ya mwanzo ya ukokotozi wa nomino [ i dé fe]. Pia, baada ya utekelezwaji wa kanuni ya 1, hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa imetekelezwa katika hatua iliyofuata kabla ya utekelezwaji wa hatua ya mwisho ya Sharti la Ukubalifu katika ukokotozi wa uibuzi wa toni katika nomino [ i dé fe]. Kutokana na matokeo ya ukokotozi wa data ya 1(a) kukubalika, kanuni hiyo hiyo itatumika kukokotoa data (1b) na matokeo yake yatakuwa sahihi. Hivyo, hatuna budi kuendelea na uchanganuzi wa tabia ya ujitokezaji wa toni katika kundi la pili la nomino za silabi mbili kama data (2) inavyoonekana hapa chini:

2.
- a) i k mú rya 'Kijinga cha moto kikubwa'
- b) i k dí di 'kijiji kikubwa'
- c) i k té nde 'mguu mkubwa'

d) i k dé ngu 'kiti kikubwa'
e) i k fú fu 'mlima mkubwa'
f) i k fá sha 'kiwanja kubwa'
g) i k dí ngo 'kichane cha ndizi kikubwa'
h) i k fí ryi 'kipekecheo kikubwa'

Tukichunguza kwa umakini data (2) hapo juu, tunaweza kubainisha masuala ya kimofolojia na kitoni kama ifuatavyo: Kimofolojia tunaona kwamba nomino zote katika 2(a-h) zina viambishi viwili ambavyo ni kiambishi awali kitangulizi /i-/ na kiambishi awali /-k-/. Kila kiambishi kina kazi yake katika nomino za data (2) hapo juu, yaani, kiambishi /i-/ pamoja na kufanya kazi ya kuwa kiambishi awali kitangulizi, pia hufanya kazi ya ukubwashaji wa nomino, ambapo hali hiyo hutokea iwapo na iwapo tu KAK imeambatana na KA katika nomino moja. Yafaa ieleweke kuwa katika Kirombo, kabla ya upachikwaji wa kiambishi /i-/, nomino zote katika (2) zilikuwa zinaanza kwa kiambishi awali /k-/ pekee na maana ya nomino hizo ni ya kawaida pasi kuwa na sifa ya ukubwa. Kwa mfano nomino zifuatazo zina KA pekee na maana yake ni ya kwawaida:

a) k dí di 'kijiji
b) k té nde 'mguu
c) k dé ngu 'kiti

Ila baada ya kupachikwa kiambishi awali kitangulizi /i-/ ambacho ndicho hufanya kazi ya ukubwashaji wa nomino katika Kirombo, maana ya nomino hizo hubadilika na kuwa na sifa ya ukubwa kama inavyoonekana hapa chini:

a) **i-** k dí di 'kijiji kikubwa'
b) **i** -k té nde 'mguu mkubwa'
c) **i** -k dé ngu 'kiti kikubwa'

Mbili, kiambishi /-k-/ hufanya kazi kama kiambishi awali cha nomino katika data (84) hapo juu. Yafaa ikumbukwe kuwa ilishaelezwa kwamba, katika Kirombo kuna udondoshaji wa irabu kulingana na mazingira ya utokeaji kifonolojia. Hivyo, kiambishi awali /-k-/ mwanzo kilikuwa na irabu /-i-/ ambacho kutokana na michakato ya kifonolojia kimedondoshwa katika mazingira ya kutanguliwa na konsonanti /k-/ na kufuatiwa na konsonanti za *ufizi, midomo* na *midomo meno* kama inavyoonekana katika (2). Irabu /-i-/ ambayo ni irabu ya juu mbele hudondoshwa katika utamkaji wa wazungumzaji wa Kirombo, kwa sababu ya urahisishaji wa matamshi.

Pia, kimofolojia data (2) inaonekana kuwa na idadi sawa ya silabi mbili katika mashina ya nomino. Aidha, muundo wa mfuatano wa silabi ya kwanza ya shina katika nomino za data (2) hulandana isipokuwa silabi za mwisho za shina ambazo huishia na ama KI katika 2(b,c na f), KKI katika 2(d,e,g na h) au KyI katika 2(a na i). Hata hivyo, tofauti za kimuundo katika silabi ya mwisho ya shina katika (2) haileteleze tofauti za kitoni kwa sababu zote zina toni C.

Ili suala la ukubwashaji linalofanywa na KAK liweze kueleweka vizuri yafaa tuchunguze kwa kulinganisha data (2) dhidi ya data (1) hapa chini:

1. a) i dé fe 'debe'
b) i kó sha 'jani la mgomba'
c) i kú mbi 'kienge'
d) i kú nya 'gunia'
e) i sá ka 'pori'
f) i bí ba 'pipa'

Linganisha na data (2) hapa chini:

2. a) i k mú rya 'Kijinga cha moto kikubwa'
b) i k dí di 'kijiji kikubwa'
c) i k té nde 'mguu mkubwa'
d) i k dé ngu 'kiti kikubwa'
e) i k fú fu 'mlima mkubwa'
f) i k fá sha 'kiwanja kubwa'
g) i k dí ngo 'kichane cha ndizi kikubwa'
h) i k fí ryi 'kipekecheo kikubwa'

Ukichunguza kwa umakini data (1) dhidi ya data (2) hapo juu, utagundua kwamba kiambishi / i- / katika data (1) hujitokeza kama kiambishi awali (KA) na hakuna sifa ya nomino inayojitokeza katika data hiyo. Aidha, irabu hiyo hiyo katika data (2) hujitokeza kama KAK, kisha kufuatiwa na KA ambayo huwakilishwa na konsonanti / -k-/. Alkadhalika, ukiondoa kiambishi awali kitangulizi { i- } katika data (2) hapo juu sifa ya nomino hizo haibaki katika nomino hizo, kwa mfano;

a) _*klyiko* ‘kijiko’,
b) _*kdidi* ‘kijiji’,
c) _*ktende* ‘mguu’,
d) _*kdingo* ‘kichane’

Kwa hakika, nomino (a-d) hapo juu, zinaonesha wazi kwamba, kiambishi awali kitangulizi { i- } kikidondoshwa, sifa ya nomino inayohusishwa nayo pia hupotea. Hali hii inadhibitisha kwa uwazi kwamba, nomino za Kirombo huwa na kivumishi ndani yake ambacho huwakilishwa na KAK na ambacho hakijitokezi kiupekee katika nomino wakati wa usemaji kwa wazungumzaji wa Kirombo kama inavyoonekana katika data (2) hapo juu.

Kabla ya kuendelea na uchanganuzi wa tabia ya toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za kundi la pili, yafaa tuweke bayana kwa kufafanua lau kwa undani mambo ya kimofolojia tuliyoyabainisha katika (2) hapo juu. Tukianza na suala la udondoshaji wa irabu, yafaa ieleweke kwamba, udondoshaji wa irabu /i/ ni hali ya kuondoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi au neno. Hali hii hutokana na sauti moja kuathiri sauti nyingine, hivi kwamba ili neno lifuate muundo unaokubalika katika lugha husika, sauti moja hulazimika kuachwa au kudondoshwa. Udondoshaji katika Kirombo hujitokeza katika aina za maneno kama nomino na kivumishi. Katika data (2) udondoshaji uliotokea ni wa irabu / i/ katika nomino na ambao utawaliwa na kanuni maalumu kama ifuatavyo:

**Kanuni 2 ya Udondoshaji wa irabu / i/**

/ i / ⟶ [ ø] / _K (konsonanti halisi za ufizi, midomo na midomo meno)

Kanuni ya (02) hapo juu inasomeka kuwa, irabu / i / hudondoshwa na kuwa kapa katika mazingira ya kufuatiwa na konsonanti halisi za ufizi, midomo na midomo meno.

Pia, yafaa ieleweke kuwa, katika lugha ya Kirombo udondoshwaji wa irabu / i / hutokea iwapo na iwapo tu, konsonanti inayoitangulia irabu hiyo ni / k /. Aidha, tunapenda kutanabaisha kuwa, udondoshaji wa irabu hautokei katika Kirombo, iwapo nazali /m/ hufuatiwa na irabu / a, e na o /. Pia, konsonanti / k / ikifuatiwa na irabu / u / udondoshaji hautokei hata kama irabu hiyo itafuatiwa na konsonanti halisi ya ufizi. Kwa mfano nomino *ik**u**dúlya* ‘gudulia’, si kwa irabu / u / pekee bali pia kwa irabu / a, o na e / zikitanguliwa na konsonanti / k / huwa hazidondoshwi katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo. Kwa mfano katika nomino kama:

*a) ik**ó**sha* ‘ jani la mgomba’,
*b) ik**á**sha* ‘ ganda la kunde au kiberiti’,
*c) ik**é**sa* ‘jiwe la kusagia ulezi au mtama’

Sanjari na hayo, tukitazama kwa undani data (2) tunaweza kuainisha masuala ya kitoni kama ifuatavyo: Nomino za data (2) zina toni J moja na toni C tatu ambazo ndizo hufanya kundi la pili la nomino za silabi mbili za shina kuwa na tabia ya ujitokezaji wa toni ya CCJC. Yaani, kulingana na data (2) KAK na KA zote huhusishwa na toni C katika Kirombo, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino za (2). Kanuni za toni zitakazotumika kukokotoa uibuzi wa toni katika kundi hili ni zile zile za kundi la kwanza.

Baada ya kutoa ufafanuzi huo, sasa tunaweza kuendelea na ukokotozi wetu wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani katika (2) hapa chini:

i k mú rya ‘Kijinga cha moto kikubwa’

/i k mu rya/ ‘Umbo la ndani’

J

2. i k mu rya ‘Upachikaji wa TJM’

C J C

i k mu rya ‘Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa’

C C J C

i k mu rya ‘Sharti la Ukubalifu’

[i k mú rya] 'Umbo la nje'

Katika ukokotozi wa 2 hapo juu, tumepata matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [i k mú rya]. Matokeo ya ukokotozi (2) yanaonesha kwamba, tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino [i k mú rya] ni CCJC. Yaani, tabia ya toni huanza kwa toni C katika KAK, ikifuatiwa na toni C katika KA, ambayo pia hufuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino [i k mú rya]. Aidha, tukichunguza kwa umakini ukokotozi wa nomino [i k mú rya] katika (2) hapo juu, tunagundua kwamba kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM kwenye silabi ya kwanza ya shina imetekelezwa kabla ya utekelezwaji wa hatua ya uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa. Katika hatua ya mwisho ya ukokotozi wa nomino [i k mú rya], imetekelezwa kanuni ya Sharti la ukubalifu kama inavyodaiwa na nadharia ya FVH.

Matokeo ya ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za silabi mbili katika Kirombo yanalandana kwa kiasi kikubwa na matokeo ya Kivenda hususani kwa nomino za silabi mbili zenye KA kama vile *mu-sé-lwa* 'bride', *mu-sádzi* 'woman'(Casemjee, 1986:15). Ujitokezaji huo wa toni katika Kivenda hulandana na ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi mbili za shina za Kirombo. Hata hivyo, inaonekana Kivenda kina nomino zenye toni C pekee bila toni J katika shina kama vile *mu-tuka* 'youth' na Kivenda pia kina nomino za silabi mbili ambazo zina toni J katika silabi ya mwisho kama vile *mu-rathú*. Ujitokezaji wa tabia ya toni wa aina hizi mbili za mwisho katika Kivenda husigana kwa kiwango kikubwa na ule wa Kirombo kwa sababu Kirombo hakiruhusu toni J kujitokeza katika silabi ya mwisho ya shina na hakina nomino yenye toni C pekee. Hivyo, hizo ni tofauti za Kitoni zinazoweza kutofautisha lugha ya Kivenda na Kirombo kwa sababu kila lugha ina tabia yake ya ujitokezaji wa toni kulingana na sifa za vipengee vyake vya lugha husika kiisimu.

Aidha, katika ukokotozi (2), kanuni za toni katika ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani zimezingatiwa kwa kuanza na kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina ambayo imefuatiwa na hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa ambayo imefuatiwa na hatua ya utekelezaji wa Sharti la Ukubalifu mwishoni mwa ukokotozi wa nomino [i k dí di] kama inavyoonekana katika (2) hapo juu. Kulingana na matokeo ya ukokotozi ya uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani katika (2) kukubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo, tunaweza kuendelea na uchanganuzi wa tabia za ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino zenye idadi ya silabi tatu za shina.

**5.2 Ujitokezaji wa Tabia za Toni katika Nomino za Silabi tatu za Shina**

Baada ya kujadili ruwaza za ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi mbili, sasa tuangazie nomino za silabi tatu katika Kirombo. Kutokana na data ya utafiti, tumegundua kwamba tabia za ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi tatu zipo katika makundi matatu tofauti ambayo ni: CJJC, CCJJC na CJC. Tuanze kwa kuchanganua ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika kundi la kwanza la CJJC kama inavyoonekana katika 7 hapa chini:

| | |
|---|---|
| 7. a) i tú lú ku | 'kisiki' |
| b) i tó ngó ti | 'gunzi' |
| c) i kó jó rho | 'godoro' |
| d) i dí ryí sha | 'dirisha' |
| e) i ká ryá i | 'beseni' |
| f) ma é ngé rye | 'miti ya maji ya mbuzi' |
| g) ma bá bá i | 'mapapai' |
| h) ma dé ngé u | 'kunde' |

Tukitazama kwa umakini data (7) hapo juu tunaweza kubainisha masuala mbalimbali ya kimofolojia na kitoni kama ifuatavyo: Kimofolojia, nomino za data (7) zina idadi sawa ya silabi za shina ambazo ni tatu na zimejitokeza kwa maumbo tofautitofauti. Hutokeaji wa silabi za shina la nomino katika (7) unaonekana kuwa, silabi ya kwanza ya shina katika 7(a – e) hulandana kwa kuwa na muundo wa KI isipokuwa katika 7(g) ambayo ina muundo wa irabu pekee. Ila silabi ya pili na ya mwisho wa shina hutofautiana kwa sababu nyingine zina muundo wa KI, KKI na nyingine zina muundo wa irabu pekee kama inavyoonekana katika 7(f na g). Tofauti za maumbo ya silabi hazileteleziathari katika za utokeaji wa tabia ya toni. Pia, nomino za (7) zimeanza kwa viambishi /i-/ na /ma-/. Kiambishi /i-/ ni kiambishi awali, kinachowakilisha hali ya umoja wa nomino katika 7(a – e), wakatika /ma-/ ni kiambishi awali kinachowakilisha hali ya uwingi wa nomino katika 7(f – h).


Aidha, kitoni nomino za silabi tatu za shina katika (7) zina toni J mbili na toni C mbili ambapo ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika nomino hizo huanza kwa toni C katika KA, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina ambayo pia hufuatiwa na toni J nyingine katika silabi ya pili ya shina na kisha kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Jambo la kujiuliza hapa ni kwamba, kwanini kuna toni J mbili katika shina la nomino

zilizopo katika (7) hapo juu? Je, hizo ni toni J mbili tofauti au ni toni J ile ile ya silabi ya kwanza ya shina inajirudia katika silabi ya pili ya shina la nomino hizo?

Hapa tunapaswa tujiridhishe kuwa utokeaji wa toni J mbili kwenye mashina ya nomino katika (7) ni ujirudiaji au laah! Ukitazama data (7) kwa umakini utaona kuwa toni J iliyojitokeza katika silabi ya kwanza ya shina ndiyo hiyo hiyo (inafanana) iliyojitokeza tena kwenye silabi ya pili ya shina la nomino husika. Hivyo, inawezekana kuwa toni J ya silabi ya kwanza ya shina imejirudia katika silabi ya pili ya shina. Pia, inawezekana kuchukulia kwamba katika mashina ya nomino za (7) kuna toni J mbili tofauti na ambazo zinaweza kuwa ni TJM mbili tofauti katika silabi mbili za shina zinazofuatana.

Aidha, kwa kuwa mkabala wa uchanganuzi wa toni kwa kutumia TJM katika nadharia ya FVH utumia toni J kama msingi wa uchanganuzi, na kwa kuwa katika Kirombo TJM upachikwa katika silabi ya kwanza ya shina basi tunachukulia kwamba katika nomino za data (7) kuna TJM mbili kwa sababu zimejitokeza katika silabi mbili tofauti ingawa zinafuatana. Hata hivyo, tukichunguza kwa umakini nomino za silabi tatu za shina katika data (7), tunagundua kwamba katika utamkwaji wake, kuna mzunguko mmoja tu wa kiimbotoni. Yaani, hakuna ujirudiaji wa mzunguko mmoja wa kiimbotoni katika usemaji ambao kitoni ungeweza kutupatia viimbotoni msingi viwili, ambavyo kwa upande wa mkabala wa tonijuu msingi katika nadharia ya FVH tungesema kuwa kuna TJM mbili. Hivyo, kutokana na maelezo hayo ya kinadharia, tunapendekeza TJM ya silabi ya pili ya shina idondoshwe kwa kuwa imeshagundulika kuwa hakuna TJM mbili katika nomino za silabi tatu za shina. Katika kutekeleza mchakato wa udondoshaji wa TJM ya shina, tunaweza kuchonga kanuni ya udondoshaji wa TJM hapa chini:

**Kanuni ya 2; udondoshaji wa TJM ya shina la nomino.**




Kanuni ya 2 hapo juu inasema kuwa, ikiwa kuna TJM mbili zinazojitokeza katika silabi mbili za shina la nomino na ambazo zinazofuatana, basi ile TJM ya pili inayojitokeza katika silabi ya pili ya shina inapaswa idondoshwe ili kuruhusu kanuni ya msambao wa toni J kufanya kazi. Hebu tuchunguze ukokotozi kwa kutumia kanuni ya 2 ya udondoshaji wa TJM ya shina la nomino katika 7 hapa chini:

i tú lú ku 'kisiki'
/i tu lu ku/ 'Umbo la ndani'

J J

7. i tu lu ku 'Upachikaji wa TJM'

J

i tu lu ku 'Udondoshaji wa TJM ya silabi ya pili.

C J C

i t u lu ku 'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa'

C J C C

i tu lu ku 'Sharti la Ukubalifu'

[*i tú lu ku] 'Umbo la nje'

Ukokotozi wa (7) hapo juu, umetupatia matokeo yasiyokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [*i tú lu ku]. Matokeo ya ukokotozi (7) yanaonesha kwamba kuna toni J moja tu ambayo imejitokeza katika silabi ya kwanza ya shina pekee. Hivyo, silabi nyingine pamoja na kiambishi awali zimebeba toni C. Ukichunguza kwa umakini ukokotozi wa 7 utagundua kwamba, kanuni ya udondoshaji wa TJM ya pili imetekelezwa baada ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina kama kanuni ya kwanza ya upachikaji wa TJM katika silabi

ya kwanza ya shina inavyohitajia. Hata hivyo, baada ya udondoshaji wa TJM ya pili, silabi iliyohusishwa nayo imebaki bila toni. Ila, kwa kuwa tulikwisha sema kwamba kitamkwa ambacho hakijaalamishwa huchukuliwa kuwa kina toni chini, basi moja kwa moja silabi ya pili ya shina itakuwa na toni C. Katika utekelezaji wa hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa, toni C ya silabi ya mwisho ya shina la nomino [*i tú lu ku] imehusishwa pia na silabi ya pili ya shina ambayo toni J yake imedondoshwa.

Kutokana na matokeo ya ukokotozi wa 7 ambayo yametumia kanuni ya 2 ya udondoshaji wa TJM ya shina la nomino tuliyoichonga hapo juu, tunapata ukweli kwamba haiwezekani kuwa nomino katika (7) zina TJM mbili na kama ndivyo, hakuna udondoshwaji wa TJM unaojitokeza na hivyo kanuni ya 2 ya udondoshaji wa TJM iliyochongwa haiwezi kutupatia matokeo sahihi. Pia, haiwezi kuwa sahihi kuhusisha toni C ya silabi ya mwisho ya shina na silabi ya pili ambayo toni J yake imedondoshwa, kwa sababu tukichukulia kuwa kila kitamkwa ambacho hakijaalamishwa moja kwa moja kichukuliwe kina toni C, itakuwa ni uhamuzi wa haraka sana, kwani tutapaswa kujiuliza tena kuwa toni J iliyodondoshwa katika silabi ya pili ya shina imeenda wapi? Je, inawezekana baada ya kanuni ya udondoshaji kitamkwa kilichokuwa na toni J kihusishwe na toni C? Je, katika Kirombo kuna uwezekano wa toni C ya kulia kujirudia kwa kuelekea kushoto? Hapa jibu la swali la pili na la tatu ni kwamba haiwezekani. Pia, jibu la swali la kwanza ni kwamba haifahamiki toni J hiyo imekwenda wapi. Hivyo, tunapaswa kuitazama upya data 7 ili kujua ni kwa nini nomino hizo zina toni J mbili?

Aidha, ukweli tulioubaini katika data (7) ni kwamba, hakuna TJM mbili, bali kuna ujirudiaji wa toni J ya silabi ya kwanza ya shina unaojitokeza kuelekea kulia mwa shina la nomino. Kwa hali hiyo, udondoshaji wa TJM ya shina ulitokea ili kuondoa dhana ya kuwa na TJM mbili katika silabi za shina moja zinazofuatana na hivyo kuruhusu toni J ya kwanza ya shina ijirudie katika silabi ya pili ya shina. Hali ya ujirudiaji wa toni kuelekea kulia au kushoto mwa shina kitoni huitwa *msambao wa toni*. Hivyo, toni J ya silabi ya kwanza ya shina husambaa kuelekea kulia mwa shina la nomino na siyo kwamba ni toni J mbili tofauti. Kutokana na ujithihirishaji wa tabia ya msambao wa toni J, tuliona kuna haja ya kuunda kanuni iliyotusadia katika ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za silabi tatu za shina kama inavyoonekana katika kanuni (3) hapa chini:

Kanuni ya 3: **Msambao wa Tonijuu katika Nomino**





Kanuni (3) inasomeka kuwa, tonijuu inasambaa kuelekea kulia mwa shina la nomino, ikiwa na maana kuwa tonijuu huanzia silabi ya kwanza ya shina hadi ama silabi ya mwisho kasoro mbili au moja kutoka mwishoni mwa shina la nomino.


Kutokana na kanuni (3) tunaweza kukokotoa nomino za silabi tatu za shina zilizopo katika (7) kwa kutumia nomino *i tú lú ku* 'kisiki'hapo juu, kama ifuatavyo:

i tú lú ku 'kisiki'


/i tu lu ku/ 'Umbo la ndani'

7. 

'Upachikaji wa TJM'



'Usambaaji wa TJM'



'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa'

C J J C

| | | |

i tu lu ku 'Sharti la Ukubalifu'

[i tú lú ku] 'Umbo la nje'

Ukokotozi wa (7) hapo juu umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [i tú lú ku]. Ukichunguza matokeo ya ukokotozi 7 utaona kwamba ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino [i tú lú ku], huanza kwa toni C katika KA, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo husambaa hadi kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya pili ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Aidha, katika ukokotozi wa (7), kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM imetekelezwa katika hatua ya mwanzo kwa kupachikwa katika silabi ya kwanza ya shina. Pia, kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina la nomino imetekelezwa kabla ya utekelezaji wa hatua ya uhusishaji wa Tonichini na vitamkwa. Aidha, Sharti la Ukubalifu limetekelezwa katika hatua ya mwisho ya ukokotozi wa uibuzi wa toni katika nomino [i tú lú ku] kama inavyoelezwa na nadharia ya FVH.

Kulingana na matokeo ya ukokotozi wa mfano wa data (7) hapo juu, tunaweza kuhitimisha kwamba nomino za silabi tatu za shina zina msambao wa toni J ambao hutawaliwa na kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina la nomino katika Kirombo. Hivyo hatuna budi kuendelea na uchanganuzi wa ruwaza ya toni katika kundi la pili la nomino za silabi tatu za shina kama ifuatavyo:

Kundi la pili la nomino za silabi tatu za shina ni lile lenye ruwaza ya ujitokezaji wa toni wa CCJJC. Hebu tuchunguze data (8) kama inavyoonekana hapa chini:

8. a) i mu mbá lá sho 'mbaazi kubwa'
b) i mu mbó ryí ko 'bakuli kubwa'
c) i ki á mbá sa 'ukuta mkubwa'
d) i mu é ngé rye 'mti mkubwa wa majani ya mbuzi'
e) ka k pá mbá sa 'ukuta mdogo'
f) i k bó bó ryi 'panyabuku mkubwa'
g) i mu sé sé fe 'mti wa dawa ya kuchachusha mbege'
h) i mu sú má ryi 'msumari mkubwa'

Tukichunguza kwa umakini data (8) hapo juu, tunaweza kubainisha masuala ya kimofolojia na kitoni kama ifuatavyo: Kimofolojia, nomino za data (8) zina idadi sawa ya silabi za shina ambazo ni tatu na zimejitokeza kwa maumbo tofautitofauti. Aidha, silabi ya kwanza ya shina katika nomino za 8(a na b) zina muundo sawa wa KKI, zile za 8(c na d) nazo zina muundo sawa wa irabu pekee, wakati zile za 8(e,f,g na h) muundo wake ni wa KI. Maumbo na muundo wa silabi ya pili na ya tatu za shina la nomino za (8) hutofautiana, ingawa tofauti hizo hazileteleza tofauti za ujitokezaji wa tabia ya toni katika nomino hizo. Pia, yafaa ieleweke vyema kwamba, viyeyusho vinavyoonekana kama kijenzi mojawapo cha baadhi ya silabi katika nomino za (8), kifonolojia havijatokana na mchakato wa uyeyushaji bali ni asili ya silabi za nomino hizo katika Kirombo. pia, nomino za (8) hapo juu zimeundwa kwa viambishi viwili ambavyo ni; kiambishi awali Kitangulizi (KAK) na kiambishi awali (KA). Katika nomino za (8) KAK zilizopo ni /i-/ ambayo hufanya pia kazi ya ukubwashaji wa nomino kama ilivyofafanuliwa mwanzo katika nomino za silabi mbili za shina na /ka-/ ambayo nayo pia hufanya kazi ya udogoshaji kama ilivyoelezwa pia katika nomino za silabi mbili za shina. Pia, KA zilizopo ni /-mu-/ /-ki-/, Ila nomino za 8(e na f) zina KA ambayo ni /-K-/ pekee kutokana na mchakato wa udondoshaji uliojitokeza wakati wa utamkaji, kwa sababu awali ilikuwa /ku/ na kubadilika kuwa [k-] ambapo irabu /-u-/ hudondoshwa katika mazingira ya kutanguliwa na konsonanti /k-/ na kufuatiwa na konsonanti halisi ya midomo /-p/ katika Kirombo.

Tukichunguza data (8) kitoni, tunaweza kubainisha masuala yafuatayo: Moja, kuna toni J mbili katika shina ambazo zimejitokeza katika silabi ya kwanza na ya pili ya shina na kuna toni C tatu ambazo zinajitokeza katika KAK, KA, na katika silabi ya mwisho ya shina. Ujitokezaji huo wa toni ndio unaofanya nomino za (8) kuwa na ujitokezaji wa tabia ya toni ya CCJJC. Ikiwa na maana kuwa ujitokezaji wa toni huanza kwa toni C ambayo hujitokeza katika KAK, ikifuatiwa na toni C ya KA, kisha kufuatiwa na toni J ya silabi ya kwanza ya shina na ambayo usambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya pili kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina katika nomino za (8). Hebu tuchunguza ukokotozi wa uibuzi wa toni katika (8) hapa chini:

**i mu sú má ryi 'msumari mkubwa'**

/ i mu su ma ry/ 'Umbo la ndani'

J

8. i m su ma ryi ‘Upachikaji wa TJM’

J

i m su ma ryi ‘Usambaaji wa TJM’

C J C

i m su ma ryi ‘Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa’

C C J J C

i m su ma ryi ‘Sharti la Ukubalifu’

[i m sú má ryi] ‘Umbo la nje’

Ukokotozi wa (8) hapo juu, umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [i m sú má ryi]. Matoko ya ukokotozi wa (8) yanaonesha kwamba, tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino [i m sú má ryi], huanza kwa toni C katika KAK, ikifuatiwa na toni C katika KA, kisha kufuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo usamabaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya pili ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino [i m sú má ryi]. Aidha, utaratibu wa utumizi wa kanuni za ukokotozi wa uibuzi wa toni kimpangilio umezingatiwa hatua kwa hatua ambapo, kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina imetekelezwa katika hatua ya mwanzo, ikifuatiwa na kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina la nomino [i m sú má ryi] kabla ya utekelezaji wa hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa. Mwisho, imetekelezwa kanuni ya sharti la Ukubalifu katika ukokotozi wa nomino [i m sú má ryi] kama inavyodaiwa na nadharia ya FVH.

Kwa kuwa matokeo ya ukokotozi katika (8) yanakubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo, hatuna budi kuendelea na uchanganuzi wa ruwazaya ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la kundi la tatu la nomino za silabi tatu za shina kama ifuatavyo:

Kabla ya kuchunguza data ya kundi la tatu la nomino za silabi tatu za shina, yafaa ifahamike kwamba kulingana na data ya utafiti, tumegundua kundi la tatu la nomino za silabi tatu za shina halina viambishi, ama vya KAK au vya KA kabisa. Pia, ikumbukwe ilielezwa kwamba TJM huhusishwa na silabi ya kwanza ya shina, jambo hilo linaonekana tofauti katika kundi hili, kwani TJM uhama kutoka silabi ya kwanza ya shina na kuhusishwa na silabi ya pili ya shina. Aidha, imebainika kuwa tabia ya ujitokezaji wa toni katika kundi la tatu la nomino za silabi tatu ni CJC. Tuchunguze data (9) hapa chini:

9. a) fa fí je ‘mjomba’
b) se sé ni ‘mdudu anayekata mimea
c) mi mí na ‘nyumba ya suti la tope’
d) me ngé le ‘kichumi’
e) nde ng’á so ‘laana’
f) nde ké rye ‘pumbu’
h) sha ngá si ‘shangazi’
i) sho ryó ko ‘choroko’
j) ngu ryá ni ‘majivu’

Tukitazama data ya (9) kwa umakini tunaweza kubainisha mambo yafuatayo: Moja, nomino zote katika (9) hapo juu, zina idadi sawa ya silabi tatu za shina ingawa zina maumbo na miundo tofauti ya hutokeaji wa silabi za shina. Tofauti za utokeaji wa maumbo na miundo ya silabi za shina haziletelezi athari za ujitokezaji wa ruwaza ya toni katika nomino za silabi tatu za shina katika (9). Pia, tukichunguza kwa umakini nomino katika (9) tunagundua kwamba, nomino zilizopo kwenye data (9) hazina viambishi ama vya KAK au vya KA. Aidha, kitoni data (9) inaonesha kwamba, ina toni J moja na toni C mbili ambapo hali ya utokeaji huo wa toni ndio unaoleteleza ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi tatu za shina kuwa CJC. Yaani, silabi ya kwanza ya shina ina toni C, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya pili pekee, ikifuatiwa na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino husika. Hivyo, kulingana na data (9), tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino za kundi la tatu la nomino za


silabi tatu za shina ni CJC. Hebu tuchunguze ukokotozi wa uibuzi wa toni kwenye umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino *sho ryó ko* ‘choroko’katika 9 hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| | sho ryó ko | ‘choroko’ |
| | /sho ryo ko/ | ‘Umbo la ndani’ |
| 9. | J<br>sho ryo ko | ‘Upachikaji wa TJM’ |
| | J<br>sho ryo ko | ‘Usambaaji wa TJM’ |
| | J C<br>sho ryo ko | ‘Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa’ |
| | J J C<br>sho ryo ko | ‘Sharti la Ukubalifu’ |
| | *[shǒ ryo ko] | ‘Umbo la nje’ |

Ukitazama kwa jicho la haraka ukokotozi wa data (9) hapo juu, hasa katika hatua ya kwanza ya utekelezaji wa kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina na hatua ya pili ya utekelezaji wa kanuni ya msambao wa TJM kuelekea kulia, unaweza kuhitimisha kwa haraka kuwa matokeo ya ukokotozi (9) ni sahihi. Ila ukweli ni kwamba matokeo ya ukokotozi wa (9) hapo juu si sahihi na hayakubaliki katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo *[*shǒ ryo ko*]. Ukichunguza kwa umakini ukokotozi (9) hapo juu, utaona kwamba silabi ya kwanza ya shina imehusishwa na toni J hali ambayo si sahihi na ni tofauti na inavyoonekana katika data (9) kabla ya ukokotozi ambapo silabi hiyo ilikuwa na toni C. hivyo, hali ya silabi ya kwanza ya shina kuwa na toni J imeleteleza matokeo tofauti na yasiyokubalika katika usemaji wa wazungumzaji Kirombo *[*shǒ ryo ko*].

Aidha, matokeo hayo yanahashiria kwamba, kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina la nomino kama ilivyoelezwa awali, haifanyi kazi katika nomino za (9). Hii ni kwa sababu toni J imehama na kujitokeza katika silabi ya pili ya shina na hivyo kufanya silabi ya kwanza ya shina kuwa na toni C. Pia, matokeo (9) yanaonesha kuwa, kanuni ya msambao wa TJM kuelekea kulia mwa shina haiwezi kufanya kazi kwenye mifano ya nomino za kundi la tatu kwa sababu toni J iliyopo kwenye silabi ya pili ya shina haionekani kusambaa. Hivyo, tunalazimika kuunda kanuni nyingine mwafaka katika kushughulikia ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika kundi la tatu la nomino za silabi tatu za shina. ili kutekeleza hilo, tumependekeza kutumia kanuni ya *Uhamaji wa TJM*. Katika kutekeleza kanuni hii, sharti silabi ya kwanza ya shina ihusishwe na toni J kabla ya kuihamisha kwenda silabi ya pili ya shina na kabla ya utekelezaji wa hatua ya uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa. Tuchunguze kanuni (4) ya uhamaji wa TJM kutoka silabi ya kwanza ya shina kwenda silabi ya pili ya shina kama inavyoonekana hapa chini:

Kanuni ya 4 ya Uhamaji wa TJM kutoka silabi ya kwanza ya shina.



Zingatia: Alama ya [ **$** ] katika kanuni 4 hapo juu ina maanisha silabi.
Hivyo, kanuni 4 inasomeka kuwa, TJM ihamishwe kutoka silabi ya kwanza ya shina kwenda silabi ya pili ya shina kwa nomino zisizokuwa na viambishi ama vya KAK au vya KA katika nomino za Kirombo.

Sasa kwa kutumia kanuni ya 4 hapo juu na kanuni nyingine za toni, tunaweza kukokotoa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino *sho ryó ko* 'choroko' kama inavyoonekana katika (9) hapa chini:

Sho ryó ko — 'choroko'
/sho ryo ko/ — 'Umbo la nje'

J

9. sho ryo ko — 'Upachikaji wa TJM'

J J

sho ryo ko — 'Uhamaji wa TJM'

J

sho ryo ko — 'Upachikaji wa TJM'

C J C

sho ryo ko — 'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa'

[sho ryó ko] — 'Umbo la nje'

Ukokotozi katika (9) hapo juu, umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [sho ryó ko]. Matokeo yanaonesha kwamba, tabia ya ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino [sho ryó ko], huanza kwa toni C katika silabi ya kwanza ya shina, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya pili ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Pamoja na matokeo ya (9) kukubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo, ukokotozi (9) umezingatia utaratibu wa utumizi wa kanuni za toni kimpangilio kwa kuanza na kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina, ikifuatiwa na kanuni ya uhamaji wa toni J kutoka silabi ya kwanza ya shina kwenda silabi ya pili ya shina na kufuatiwa na hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa. katika ukokotozi (9) hatuhitaji kutekeleza kanuni nyingine ya sharti la Ukubalifu kwa kuwa imeshatekelezwa katika hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa katika nomino [sho ryó ko].

Pamoja na matokeo hayo, tunaona njia ya ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za silabi tatu za shina zisizo na KAK au KA, una mzunguko mrefu ambao huhusisha kanuni na hatua nyingi kiasi ambacho kinaweza kumchanganya au kumchosha msomaji. Kwa vile tumeshagundua kwamba kundi la tatu la nomino za silabi tatu za shina katika Kirombo hazina KAK, wala KA na kuwa TJM uhamia katika silabi ya pili kutoka silabi ya kwanza ya shina, basi tunapendekeza njia nyingine fupi ambayo hatuhitaji kufuata hatua zote zilizozingatiwa katika ukokotozi wa (9) wa nomino za kundi la tatu hapo juu, utumike kama inavyoonekana katika (10) hapa chini:

na á nwa — 'ua la mgomba'

/na a nwa/ — 'Umbo la ndani'

J

10. na a nwa — 'Upachikaji wa TJM'

C J C

na a nwa — 'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa'

[na á nwa] 'Umbo la nje'

Ukokotozi katika (10) hapo juu, umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [*na á nwa*]. Matokeo ya ukokotozi (10) yanaonesha kwamba, silabi ya kwanza ya shina ina toni C, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya pili ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino [me ngé le]. Ukichunguza kwa umakini utaona kwamba, ukokotozi wa uibuzi wa toni katika (10) umezingatia hatua mbili pekee. Hatua ya kwanza ni utekelezaji wa kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya pili ya shina. Hapa inapaswa ikumbukwe kuwa, katika ukokotozi wa (9) tulikwisha gundua yakuwa TJM upachikwa kwenye silabi ya pili kwa nomino zisizokuwa na viambishi vya ama KAK au KA Kirombo (§. Kanuni ya 4) kwa maelezo zaidi. Hatua ya pili na ya mwisho katika ukokotozi (10) ni utekelezwaji wa hatua ya uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa. Katika ukokotozi (10) hatuhitaji utekelezwaji wa hatua nyingine ya Sharti la Ukubalifu kwa kuwa limekwishatekelezwa katika hatua ya pili ya ukokotozi. Hivyo, ukichunguza ukokotozi huu kwa umakini utaona tumetumia njia chache na fupi ukilinganisha na ukokotozi wa nomino katika (§. 9).

Matokeo ya ukokotozi wa nomino za silabi tatu za shina hususani nomino zisizokuwa na kiambishi katika Kirombo hushadidiwa na matokeo ya utafiti wa nomino hususani zisizokuwa na kiambishi katika Kivenda kama vile nomino [da-ná-na] 'fool' na [pha-phá-na] 'type of calabash' (Casemjee, 1986: 62). Matokeo ya hizi nomino za Kivenda yanaonesha kuwa tabia ya ujitokezaji wa toni huanza kwa toni C katika silabi ya kwanza ya shina, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya pili ya shina kisha kufuatiwa na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino za Kivenda hususani zile zisizokuwa na ama kiambishi awali kitangulizi au kiambishi awali. Hata hivyo, kuna baadhi ya nomino za silabi tatu za shina zisizo na kiambishi katika Kivenda ambazo huwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambazo huwa na msambao wa toni J kuanzia silabi ya kwanza ya shina hadi silabi ya mwisho ya shina kama vile: dá-ka-lo 'joy', khó-kho-la 'ankle-bone' na gó-ng'ó-ng'ó 'bumble bee'. Kulingana na utafiti huu, Kirombo hakina nomino za silabi tatu za shina zisizo na kiambishi zenye toni J katika silabi ya kwanza ya shia wala msambao wa toni J kutoka silabi ya kwanza hadi silabi ya mwisho ya shina.

Kutokana na matokeo hayo, mifano ya nomino iliyosalia katika kundi la tatu la nomino za silabi tatu za shina kwenye data (9) itakokotolewa kwa kuzingatia utaratibu uliotumika katika mifano ya (9 – 10) hapo juu na matokeo yake yatakuwa sahihi na yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo. Hivyo, hatuna budi kuendelea na uchanganuzi wa tabia ya ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za silabi nne za shina katika sehemu inayofuata:

### 5.3 Ujitokezaji wa Tabia za Toni katika Nomino za Silabi Nne za Shina

Baada ya kujadili kwa undani tabia za ujitokezaji wa toni katika makundi mbalimbali ya nomino za silabi tatu za shina, sasa tunaweza kuchunguza tabia za ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za silabi nne za shina. Kutokana na data ya utafiti tumegundua kuwa, tabia za ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi nne za shina zipo katika makundi matatu ambayo ni: CJJJC, CJJC na CJCJC. Tuchunguze data ya kundi la kwanza hapa chini:

| | |
|---|---|
| 11. a) i bá rí shé she | 'parachichi' |
| b) i kó í kó i | 'panya' |
| c) m kí ryí ng'á nga | 'mwiba wa uzio' |
| d) m ryí ngá ryí nga | 'mti wa mbao' |
| e) i shí mbí lyí lyi | 'minyoo ya udongoni' |
| f) k fi ní kó ni | 'chemchemi' |
| g) k só ngó mí a | 'jina la mfugaji maarufu' |
| h) ma shá ú rí yo | 'makesi hayo' |

Tukichunguza kwa umakini data (11) hapo juu, tunaweza kubainisha masuala ya kimofolojia na kitoni kama ifuatavyo: Kimofolojia tunaona kwamba, nomino za silabi nne za shina katika (11) zina viambishi awali ambavyo vina maumbo tofautitofauti kutegemea aina ya nomino yenyewe kama vile katika 11(a –c) nomino hizo zina kiambishi {i-}, katika 11(d-e) zina kiambishi awali {m-} ambacho kimetokana na mchakato wa udondoshaji wa irabu /-u-/ kuwa [ø] katika mazingira ya kufuatiwa na konsonanti halisi ya kaakaalaini /k/ na sauti ya ufizi /r/. Wakati katika 11(f- g) zina kiambishi awali {k-) ambacho kimetokana na mchakato wa udondoshaji kutoka {ku} ambapo {-u-} imekuwa kappa [ø] katika mazingira ya kufuatiwa na sauti ya ufisi /s/ na sauti ya midomo meno /f/. Viambishi awali vyote katika 11(a-g) hufanya kazi ya kuwakilisha hali ya umoja wa nomino husika. Isipokuwa kiambishi awali {ma-} cha nomino iliyopo katika 11(h) ambacho hufanya kazi ya kuwakilisha hali ya uwingi wa nomino husika. Pia, kimofolojia tunaona kuwa nomino za (11) zina idadi sawa ya silabi nne za shina ingawa


zinatofautiana kiumbo na kimuundo. Tofauti za maumbo na muundo wa silabi za nomino katika (11) hazileteleziathari katika tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino hizo.

Tukichunguza data ya 11 kitoni, tunaweza kubainisha mambo yafuatayo: kitoni nomino za silabi nne zina toni J tatu katika shina, ambazo hujitokeza kuanzia silabi ya kwanza hadi ya tatu ya shina na toni C mbili, ambapo toni C moja ni ya silabi ya mwisho ya shina wakati toni C ya pili ipo katika kiambishi awali cha nomino husika. Ujitokezaji huo wa toni ndio unaofanya kundi la kwanza la nomino za silabi nne za shina liwe na tabia ya ujitokezaji wa toni wa *CJJJC*. Yaani, ujitokezaji wa toni katika nomino za data (11) huanza kwa toni C ambayo ujitokeza katika KA, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo usambaa hadi silabi ya mwisho kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina na kisha kuishia na toni C kwenye silabi ya mwisho ya shina la nomino husika.

Kanuni ya 3 ya usambaaji wa TJM kuelekea kulia mwa shina la nomino imetumika katika ukokotozi wa uibuzi wa tabia za toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za kundi la kwanza la nomino za silabi nne za shina kama inavyoonekana katika (11) hapa chini:

i bá rí shé she ‘parachichi’

/I ba ri she she/ ‘Umbo la ndani’




[i bá rí shé she] ‘Umbo la nje’

Ukokotozi wa uibuzi wa (11) hapo juu umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kirombo [*i bá rí shé she*]. Matokeo ya ukokotozi wa (11) unaonesha kwamba, tabia ya ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino [i bá rí shé she], huanza kwa toni C katika KA, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo usambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya mwisho kasoro moja, kisha kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. Aidha, katika ukokotozi wa nomino [i bá rí shé she], kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina imetekelezwa katika hatua ya mwanzo ya ukokotozi na kufuatiwa na kanuni ya usambaaji wa toni J kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya mwisho kasoro moja ya shina. Pia, katika ukokotozi wa (11) hatua ya uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa imetekelezwa kabla ya hatua ya mwisho ya Sharti la Ukubalifu kutekelezwa. Kutokana na matokeo ya ukokotozi wa uibuzi wa toni katika 11 kukubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo, hatuna budi kuendelea na uchanganuzi wa tabia za toni katika kundi la pili la nomino za silabi nne za shina katika sehemu ifuatayo:

Kulingana na data ya utafiti tumebaini kuwa, kundi la pili la nomino za silabi nne za shina, lina tabia tofauti ya ujitokezaji wa toni ambayo ni CJJC ukilinganisha na kundi la kwanza lenye CJJJC. Hata hivyo, tofauti kubwa ya makundi haya mawili ni kwamba, nomino za kundi la pili hazina viambishi ama vya KAK au vya KA wakati kundi la kwanza lina kiambishi cha KA. Katika kundi la pili, C ya kushoto huhusishwa na silabi ya kwanza ya shina wakati katika kundi la kwanza C ya kushoto huhusishwa na KA. Pia, TJM katika kundi la pili huhusishwa na silabi ya pili ya shina wakati kundi la kwanza TJM huhusishwa na silabi ya kwanza ya shina. Hii ina maana


kuwa, utofauti wa uhusishaji wa TJM kwenye silabi za shina umetokana na uhamaji wa TJM kwenda silabi ya pili kutoka silabi ya kwanza ya shina (§. Ukokotozi wa nomino za silabi tatu za shina katika 6 na 7) kwa maelezo zaidi. Hebu sasa tuchunguze kundi la pili la nomino za silabi nne za shina kama inavyoonekana katika (12) hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| 12. | a) se ngé sé nge | 'wimbo wa tanga la mzee wa makamu' |
| | b) su sú fí ri | 'sisimizi' |
| | c) ndo kó ryó ryo | 'siafu wekundu' |
| | d) ndo ryí kó ngo | 'vumbi la udongo' |
| | e) she ké shé ke | 'chekecheke' |

Tukichunguza kwa umakini data (12) hapo juu, tunaweza kubainisha masuala kadhaa ya kimofolojia na kitoni kama ifuatavyo: Kimofolojia tunaona nomino za data (12) zina idadi sawa ya silabi nne za shina ambazo zina maumbo na muundo tofauti wa utokeaji. Kwa mfano katika 12(a na b) silabi ya kwanza ina maumbo ya konsonanti yanayolandana na zina muundo wa KI, wakati nomino zilizopo katika 12(c – e) zina maumbo tofauti ila zina muundo wa KKI ambao hulandana. Silabi zinazofuatia, yaani zile za silabi ya pili hadi ya mwisho ile ya mwisho wa shina nazo pia husigana kiumbo na kimuundo. Yafaa ieleweke kwamba, tofauti za kiumbo na kimuundo katika silabi za nomino zilizopo katika 12(a – e) haziletelezi athari katika tabia za ujitokezaji wa toni kwenye nomino hizo. Pia, kimofolojia tumegundua kwamba, kundi la pili la nomino za silabi nne za shina hazina KAK wala KA kabisa.

Kitoni, tumegundua kwamba, nomino za data 12 zina toni J mbili ambazo zimejitokeza katika silabi ya pili na ya tatu ya shina na zina toni C mbili katika shina ambazo hujitokeza katika silabi ya kwanza ya shina na katika silabi ya mwisho ya shina. Ujitokezaji wa nomino katika 12 ndio unaoleteleza tabia ya ujitokezaji wa toni katika kundi la pili la nomino za silabi nne za shina kuwa CJJC. Yaani, silabi ya kwanza ya shina ina toni C, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya pili ya shina na ambayo usambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya mwisho kasoro moja na mwisho kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino husika. Hebu tuchunguze ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za kundi la pili katika (12) hapa chini:

se ngé sé nge 'wimbo wa tanga la mzee mkubwa'
/se nge se nge/ 'Umbo la ndani'




[se ngé sé nge] 'Umbo la nje'

Katika ukokotozi wa (12) hapo juu, tumepata matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [*se ngé sé nge*]. Matokeo ya ukokotozi wa 12 yanaonesha kwamba, tabia ya ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino [se ngé sé nge], huanza kwa toni C katika silabi ya kwanza ya shina, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya pili na ya mwisho kasoro moja na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho

ya shina. Tukichunguza kwa umakini ukokotozi 12 tunagundua kwamba, kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina imetekelezwa katika hatua ya mwanzo, ikifuatiwa na kanuni ya uhamishaji wa TJM kutoka silabi ya kwanza ya shina kwenda katika silabi ya pili ya shina. Pia, tumegundua kuwa kanuni ya usambaaji wa TJM kuelekea kulia mwa shina imetekelezwa kabla ya utekelezaji wa hatua ya uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa na katika hatua ya mwisho ya ukokotozi wa nomino [se ngé sé nge] Sharti la Ukubalifu limetekelezwa.

Kulingana na matokeo ya ukokotozi wa uibuzi wa toni katika nomino za kundi la pili katika (12), kukubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo, sasa tunaweza kuendelea na uchanganuzi wa ruwaza ya toni katika kundi la tatu la nomino za silabi nne za shina katika sehemu inayofuata hapa chini;

Kutokana na data ya utafiti, tumegundua kwamba, kundi la tatu la nomino za silabi nne za shina zina ruwaza ya ujitokezaji wa toni wa CJCJC. Hebu tuchunguze data ya nomino za kundi hili katika 13 hapa chini:

13. a) i só ngo ryó ni ‘kwenye kokoto kubwa’
b) i bá ba í ni ‘kwenye papai’
c) i tú lu kú ni ‘kwenye kisiki
d) m sé se fé ni ‘katika mti wa dawa ya mbege’
e) m sá sa ngé ni ‘eneo la makutano’
f) k pá mba sé ni ‘kwenye ukuta’
g) k tí mbi ryí u ‘kwenye mwinuko’

Tukitazama kwa umakini data (13) tunaweza kubainisha mambo kadhaa ya kimofolojia na kitoni kama ifuatavyo: Kimofolojia tunaona nomino zilizopo katika data (13) hapo juu, zina viambishi awali ambavyo vimejitokeza kwa maumbo tofauti tofauti kama vile {i-}, {m-}, na {k-} kutegemeana na aina ya nomino. Pia, viambishi awali vya nomino katika (13), hufanya kazi ya kuwakilisha hali ya umoja wa nomino husika. Kiambishi {m-) ni matokeo ya mchakato wa udondoshaji wa irabu /-u-/ ambayo huwa kapa [ø] katika mazingira ya kufuatiwa na konsonanti halisi /s/ ya ufizi, wakati {k-} ni matokeo ya mchakato wa udondoshaji wa irabu /u-/ ambayo huwa kapa [ø] katika mazingira ya kufuatiwa na konsonanti halisi za midomo na ufizi /p/ na /t/. Pia, kimofolojia tunaona kuwa, nomino zote zina idadi sawa ya silabi nne za shina. Silabi za shina la nomino katika data 13 zina maumbo na muundo tofauti wa utokeaji. Kwa mfano silabi ya kwanza ya shina katika nomino zote zina idadi ya maumbo sawa na muundo wa KI, ila silabi ya pili hadi ya mwisho ya shina zina tofautiana kiumbo na kimuundo. Tofauti za kiumbo na kimuundo haziletelezi athari katika tabia ya utokeaji wa toni katika nomino za (13). Ukichunguza kwa umakini data (13) utaona kwamba silabi ya mwisho ya shina imeishia na silabi {-ni} ambayo hufanya kazi kama kiambishi tamati na kiambishi cha umahali. Silabi ya mwisho {-ni} inapojitokeza mwishoni mwa nomino za Kirombo, huathiri nomino hizo kwa kuzifanya ziwe nomino za mahali kama zinavyoonekana katika data (13). Pia, silabi ya mwisho katika 13(g) hufanya kazi kama kiambishi tamati na kama kiambishi cha umahali kama ilivyo kwa kiambishi {-ni} katika 13(a-f). Umahali unaooneshwa na kiambishi {-u} ni umahali wa sehemu ya juu ya kitu kirefu kama juu ya mlima, juu ya mti na kadhalika.

Pamoja na masuala ya kimofolojia, kitoni tunaweza kuona kuwa nomino za data (13) zina toni J mbili katika silabi za shina ambazo hazifuatani na toni C tatu ambazo pia toni C mbili ni za silabi za shina ambazo haziandamiani na toni C moja hujitokeza katika kiambishi awali. Ujitokezaji huo wa toni ndio unaofanya tabia ya ujitokezaji wa toni katika kundi la tatu la silabi nne za shina kuwa CJCJC. Yaani, toni C hujitokeza katika kiambishi awali, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina kisha kufuatiwa na toni C ambayo hujitokeza katika silabi ya pili ya shina, kisha kufuatiwa na toni J nyingine katika silabi ya tatu ya shina na kuishina na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino husika. Ujitokezaji wa ruwaza ya toni katika kundi la tatu la nomino za silabi nne za shina hutofautiana na makundi mawili yaliyotangulia katika data (11) na (12). Hii ni kwa sababu msambao wa TJM katika kundi la tatu la nomino katika (13) hutatizwa na ujitokezaji wa toni C katikati ya shina la nomino na hivyo, kufanya usambaaji usiendelee kulia mwa shina kama ilivyoonekana katika ukokotozi wa data za makundi mawili ya awali ya nomino za silabi nne za shina yaliyotangulia (§.11, na 12) kwa ufafanuzi zaidi.

Kwa kutumia kanuni za ukokotozi wa uibuzi wa toni tulizokwishaunda na ambazo zimetumika katika makundi mawili ya mwanzo ya nomino za silabi nne za shina, tuchunguze ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino i só ngo ryó ni katika 13 hapa chini:

i só ngo ryó ni 'kwenye kokoto kubwa'

/i so ngo ryo ni/ 'Umbo la ndani'

J

13. i so ngo ryo ni 'Upachikaji wa TJM'

J

i so ngo ryo ni 'Usambaaji wa TJM'

C J C

i so ngo ryo ni 'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa'

C J J J C


i so ngo ryo ni 'Sharti la Ukubalifu'

*[ i só ngó ryó ni] 'Umbo la nje'

Tukitazama matokeo ya ukokotozi wa (13) hapo juu, tunaona kwamba hayakubaliki katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo *[ i só ngó ryó ni]. Matokeo ya ukokotozi katika 13 yanaonesha kwamba, tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino *[ i só ngó ryó ni], huanza kwa toni C katika KA, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo inaonekana kusambaa hadi silabi ya mwisho kasoro moja na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho. Ukweli hapa ni kwamba, silabi ya pili ya shina imehusishwa na toni J katika matokeo hayo kimakosa kwa sababu kabla ya ukokotozi inaonekana kuwa na toni C hali inayosababisha matokeo hayo kutokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo. Pia, katika ukokotozi wa (13) utaona kuwa, kanuni ya msambao wa toni J imefanya kazi vizuri, ila matokeo yake hayakubaliki katika usemaji wa Kirombo *[ *i só ngó ryó ni*]. Hii ni kwa sababu katika msambao huo wa toni J, silabi ya pili ya shina inaonekana ina toni J katika ukokotozi (13) wakati kabla ya ukokotozi ilikuwa na toni C. Kwa sababu hii inaonesha wazi kwamba nomino *[ i só ngó ryó ni] haina msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina kwa sababu ya kuzuiliwa kwa ujitokezaji wa toni C katikati ya shina katika silabi ya pili ya shina, kisha kufuatiwa na toni J nyingine katika silabi ya tatu amabayo nayo imefuatiwa na toni C kama ruwaza ya toni (CJCJC) ya nomino katika (13) inavyoonekana.


Hivyo, katika kutatua suala la ujitokezaji wa toni katika nomino [ i só ngo ryó ni], hatuna budi kuunda kanuni nyingine itakayotuwezesha kukokotoa nomino zenye ruwaza ya ujitokezaji wa toni wa aina ya nomnio za data (13), ili kupata matokeo kubalifu. Kwa vile silabi ya pili ya shina ina toni C, na kwa kuwa imezuia mwendelezo wa usambaaji wa toni J kuelekea kulia mwa shina na kufuatiwa na toni J katika silabi ya mwisho kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino [ i só ngo ryó ni], tunaweza kuchukulia kuwa kuna ujitokezaji wa TJM mbili katika nomino za data (13). Hivyo, tunapendekeza kuunda kanuni ya *unakiliji wa TJM* itumike baada ya utekelezaji wa kanuni ya jumla ya Upachikaji wa TJM kwenye silabi ya kwanza ya shina la nomino husika.

**Kanuni ya 5 ya Unakiliji wa TJM**



Kanuni hii inasomeka kuwa, pachika TJM katika silabi ya kwanza ya shina na inakilishe katika silabi ya tatu ya shina katika nomino za kundi la tatu la nomino za silabi nne za shina zenye toni C katika silabi ya pili ya shina la nomino husika. Hebu tutumie kanuni ya 5 ya *Unakiliji wa TJM* ikitumika pamoja na kanuni nyingine za kitoni katika kufanya ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino *i só ngo ryó ni* 'kwenye kokoto kubwa' kama inavyoonekana katika (13) hapa chini:

13.




Ukokotozi wa (13) hapo juu, umetupatia matokeo yanayokubalika kulingana na usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [*i só ngo ryó ni*]. Matokeo ya ukokotozi 13 yanaonesha kwamba, ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika nomino [*i só ngo ryó ni*], huanza kwa toni C katika KA, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shinia, kisha kufuatiwa na toni C katika silabi ya pili ya shina ambayo hufuatiwa na toni J tena katika silabi ya tatu ya shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. matokeo ya ukokotozi (13) yamekubalika kwa sababu silabi ya pili ambayo ilionekana kuwa na toni J katika matokeo ya ukokotozi wa 107, kwa sasa ina toni C ambayo hushabihiana na data husika kabla ya ukokotozi (13). Aidha, tukichunguza kwa umakini ukokotozi (13) tunaona kwamba, kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM imetekelezwa kwanza kwa kupachikwa kwenye silabi ya kwanza ya shina, kabla ya utekelezaji wa kanuni ya unakiliji wa TJM katika silabi ya pili kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina. Hatua ya mwisho katika ukokotozi huu ni utekelezwaji wa hatua ya uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa. Katika ukokotozi 13 hatuhitaji kutekeleza kanuni nyingine ya utakelezaji wa Sharti la Ukubalifu kwa kuwa limekwisha tekelezwa kwenye hatua ya uhusishaji wa tonichini na vitamkwa. Hivyo, tunaweza kuendelea na uchanganuzi wa tabia za ujitokezaji wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za silabi tano za shina katika sehemu ifuatayo.

**1.4 Ujitokezaji wa Ruwaza za Toni katika Nomino za Silabi Tano za Shina**

Baada ya kujadili tabia za ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi nne za shina, sasa tunaweza kuchanganua tabia za toni katika nomino za silabi tano za shina kwa kuibua toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino hizo. Kutokana na data ya utafiti tumebaini kwamba tabia za ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi tano za shina zipo katika makundi mawili ambayo ni CCJJCJC na CJJJJC. Hebu tuanze mjadala wetu kwa kuchunguza tabia ya toni katika nomino za kundi la kwanza la CCJJCJC katika data (14) hapa chini:


14. a) i m sú má ka bú ryi 'ua linalooteshwa kaburini'
b) i m kí ryí ng'a ngé ni 'kwenye mwiba wa uzio'
c) i m sú sú fi rí ni 'kwenye sisimizi mkubwa'
d) i m bá rí she shé ni 'kwenye mparachichi mkubwa'
e) i m shí mbí lyi lyí ni 'kwenye mnyoo mkubwa'

tukichunguza kwa umakini kundi la nomino za silabi tano za shina katika (14) hapo juu, tunaweza kubainisha masuala ya kimofolojia na kitoni kama yafuatayo: Kimofolojia tunaona nomino za data ya (14) zina viambishi viwili ambavyo ni kiambishi awali kitangulizi {i-}ambacho pamoja na kuwa ni kiambishi awali kitangulizi cha nomino, pia hufanya kazi ya ukubwashaji wa nomino kama tulivyokwisha eleza awali katika uchanganuzi wa tabia za ujitokezaji wa toni kuanzia nomino za silabi mbili za shina. Kiambishi cha pili ni KA {-m-} ambacho ni matokeo ya mchakato wa udondoshaji wa irabu /u/ ambayo huwa [ø] katika mazingira ya kufuatiwa na konsonanti halisi /s/, /k/ na /b/ kama inavyoonekana katika data (14). Pia, kimofolojia tunaona kuwa, idadi ya silabi za shina katika nomino za (14) ni tano na zinalingana, ingawa hutofautiana kiumbo na kimuundo. Tulikwishasema kwamba, tofauti za silabi kiumbo na kimuundo hazileteleti athari ya ujitokezaji wa tabia ya toni katika nomino

za Kirombo. Sanjari na hayo, tulikwisha sema kwamba, kiangami {-ni} katika nomino za Kirombo hufanya kazi ya kuonesha umahali. Yaani, kinapoanjikwa kwenye nomino huathiri nomino hiyo kwa kuhifanya iwe nomino mahala.

Aidha, kitoni tunaweza kuona kwamba, katika kundi la nomino za silabi tano za shina katika (14) hapo juu, kuna toni J tatu ambazo hujitokeza katika silabi ya kwanza ya shina na kusambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya pili ya shina na toni J ya tatu imejitokeza katika silabi ya mwisho kasoro moja na kuna toni C nne ambapo mbili hujitokeza katika KAK, na KA, wakati toni C nyingine hujitokeza katika silabi ya tatu na ya mwisho wa shina la nomino husika. Ujitokezaji huo wa toni ndio unaofanya tabia ya ujitokezaji wa toni katika kundi la nomino za silabi tano za shina katika (14) kuwa CCJJCJC. Katika mifano ya nomino katika (14), silabi ya tatu ya shina ina toni C, ambayo ndiyo huzuia mwendelezo wa usambaaji wa toni J kuelekea kulia mwa shina na Kisha kufuatiwa na toni J nyingine inayojitokeza katika silabi ya mwisho kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino hizo. Katika uchanganuzi wa data ya nomino za silabi tano za shina, tumegundua kwamba, tabia ya ujitokezaji wa toni hujirudia na hivyo kuna TJM mbili zinazojitokeza katika nomino za kundi la kwanza la silabi tano za shina. Hali ya ujitokezaji wa TJM mbili katika kundi la silabi tano za shina, hushabihiana na kundi la tatu la nomino za silabi nne za shina. Hivyo, kanuni ya 5 ya unakiliji wa TJM iliyotumika pamoja na kanuni nyingine kitoni zitatumika katika ukokotozi wa uibuzi wa toni katika kundi la nomino la silabi tano za shina kama inavyoonekana katika (14) hapa chini:

i m sú má ka bú ryi ‘ua linalooteshwa kaburini’
/i m su ma ka bu ryi/ ‘Umbo la ndani’




[i m sú má ka bú ryi] ‘Umbo la nje’

Ukokotozi wa nomino katika (14) hapo juu, umetupatia matokeo yanayokubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [*i m sú má ka bú ryi*]. Ukichunguza zaidi matokeo ya ukokotozi (14) utaona kwamba, ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika nomino [i m sú má ka bú ryi] ni CCJJCJC. Yaani, KAK na KA vyote vina toni C, ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo usambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya pili ya shina, kisha toni C hujitokeza katikati ya shina kwenye silabi ya tatu ya shina na kuzuia mwendelezo wa usambaaji wa toni J kuelekea kulia mwa shina na kufuatiwa tena na toni J katika silabi ya mwisho kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina na kuishia na toni C katika silabi ya mwisho ya shina. aidha, ukitazama ukokotozi wa nomino [i m sú má ka bú ryi] utaona kwamba, kanuni ya jumla ya upachikaji wa TJM imetekelezwa kwa kupachikwa kwenye silabi ya kwanza ya shina kabla ya utekelezaji wa kanuni ya unakiliji wa TJM katika silabi ya mwisho kasoro moja. Pia, kanuni ya msambao wa TJM kuelekea kulia mwa shina imetekelezwa baada ya kanui ya unakiliji wa TJM na kabla ya utekelezaji wa hatua ya uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa. Katika ukokotozi wa uibuzi wa toni katika nomino [i m sú má ka bú ryi], utekelezwaji wa Sharti la Ukubalifu umefanyika katika hatua ya mwisho.

Baada ya kuchunguza na kuchanganua tabia ya ujitokezaji wa toni katika kundi la kwanza la nomino za silabi tano za shina, tunaweza sasa kuendelea na uchanganuzi wa tabia ya ujitokezaji wa toni katika kundi la pili la

nomino za silabi tano za shina CJJJJC. Tuanze mjadala wetu wa uchanganuzi wa tabia za kundi hili kwa kuchunguza data ya (15) hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| 15. | .a) i sú fú rí é ni | 'kwenye sufuria kubwa' |
| | b) i shá rá ndú lyé ni | 'kwenye turubali' |
| | c) i wá rí lá mó si | 'pombe ya matanga' |
| | d) i ngá shé lá rú fa | 'ndama wa mungu' |
| | e) i tí mbí ryí ú ni | 'kwenye kigongo' |

Tukichunguza data (15) kwa umakini, tunaweza kubainisha mambo kadhaa ya kimofolojia na kitoni kama ifuatavyo: tukianza na masuala ya kimofolojia, tunaona nomino za silabi tano za shina katika (15) zina kiambishi awali /i-/ ambacho pamoja na kufanya kazi ya kuwakilisha hali ya umoja wa nomino hizo, pia kinafanya kazi ya ukubwashaji wa nomino kama zinavyoonekana katika (15). Pia, nomino za data (15) zinaonekana zina idadi sawa ya silabi tano za shina, ingawa zinaonekana kuwa na maumbo na muundo unaosigana kwa namna fulani. Ikumbukwe kuwa tulishaeleza kwamba, tofauti za kiumbo na kimuundo hazina athari katika tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino za Kirombo. Pia, ilishaelezwa kwamba, kiambishi tamati {-ni} hufanya kazi ya kuonesha umahali na kinapopachikwa katika nomino huathiri nomino husika kwa kuifanya iwe nomino mahala.

Kitoni, tunaweza kuona nomino za silabi tano za shina katika (15) zina toni J nne ambazo zimejitokeza kuanzia silabi ya kwanza ya shina na kusambaa kuelekea kulia hadi silabi ya mwisho kasoro moja na kuna toni C mbili ambapo toni C moja imejitokeza katika silabi ya mwisho wa shina na toni C ya pili imejitokeza katika KA. Hali ya ujitokezaji wa toni katika data (15) ndiyo inayofanya kundi la pili la nomino za silabi tano za shina kuwa na tabia ya ujitokezaji wa toni wa CJJJJC.

Tabia ya ujitokezaji wa toni katika kundi la pili la nomino za silabi tano za shina ni tofauti na ya kundi la kwanza ambalo huwa na toni TJM mbili. Kundi la pili halina TJM mbili bali lina msambao wa toni J ambao huanzia silabi ya kwanza ya shina hadi silabi ya mwisho kasoro moja. Pamoja na kuwa zote zinaonekana kuwa na usambaaji wa J kuelekea kulia mwa shina, katika kundi la pili usambaaji wake uendelea hadi silabi ya mwisho kasoro moja kutoka mwishoni mwa shina bila kuzuiliwa na ujitokezaji wa toni C katikati ya shina kama ilivyokuwa katika kundi la kwanza kwenye data (14) na kama ilivyoonekana kwenye mifano ya ukokotozi wa uibuzi wa toni kwenye umbo la nje kutoka umbo la ndani katika (14) hapo juu. Hebu tutumie nomino [ i sú fú rí e ni] 'kwenye sufuria kubwa' kufanya ukokotozi katika (15) hapa chini:

i sú fú rí é ni 'kwenye sufuria kubwa'
/i su fu ri e ni/ 'Umbo la ndani'

J

15. i su fu ri e ni 'Upachikaji wa TJM'

J

i su fu ri e ni 'Usambaaji wa toni J'

C J C

i su fu ri e ni 'Uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa'

C J J J J C

i su fu ri e ni 'Sharti la Ukubalifu'
[ i sú fú rí é ni ] 'Umbo la nje'

Ukichunguza kwa umakini mfano wa ukokotozi katika (15) hapo juu, utaona kwamba matokeo ya ukokotozi huu ni sahihi na yanakubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo [i sú fú rí é ni]. Kutokana na matokeo ya ukokotozi katika (15), imebainika kuwa ruwaza ya ujitokezaji wa toni katika kundi la pili la nomino za silabi tano za shina ni CJJJJC. Yaani, huanza kwa toni C katika KA ikifuatiwa na toni J katika silabi ya kwanza ya shina na ambayo usambaa kuelekea kulia mwa shina hadi silabi ya mwisho kasoro moja, kisha kufuatiwa na toni C katika silabi ya mwisho ya shina la nomino [ i sú fú rí é ni ]. Aidha, ukichunguza ukokotozi (15) utagundua kuwa, kanuni ya upachikaji wa TJM imetekelezwa kwa kupachikwa katika silabi ya kwanza ya shina, kabla ya utekelezaji wa

kanuni ya msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina. Pia, hatua ya uhusishaji wa Tonichini na Vitamkwa imetekelezwa kabla ya utekelezaji wa hatua ya mwisho ya Sharti la Ukubalifu kama inavoonekana katika ukokotozi wa nomino [ i sú fú rí é ni ] hapo juu.

## Hitimisho

Matokeo ya uchanganuzi wa tabia za ujitokezaji wa toni na ukokotozi wa uibuzi wa toni katika nomino za silabi mbili za shina hadi zile za silabi tano hukubalika katika usemaji wa wazungumzaji wa Kirombo. Tumeweza kupata uelewa wa kutosha juu ya kanuni zinazotawala hutokeaji wa toni katika nomino za Kirombo. Sanjari na hayo, tumebaini kuwa ruwaza za ujitokezaji wa toni katika nomino za Kirombo zina muundo tofauti ambao hutawaliwa na kanuni ya msingi kisha kufuataiwa na kanuni nyingine za toni katika ukokotozi wa uibuzi wa toni katika umbo la nje kutoka umbo la ndani la nomino za silabi mbili hadi silabi tano za shina kama ifuatavyo:

1. Tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi mbili za shina zina muundo wa CJC ambao uchanganuliwa kwa kutumia kanuni ya msingi ya upachikaji wa TJM katika silabi ya kwanza ya shina.
2. Tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi mbili za shina zina muundo wa: a) CJJC ambao uchanganuliwa kwa kutumia kanuni ya msingi ya Msambao wa Toni J kuelekea kulia mwa shina la nomino husika.

   b) CCJJC huu ni muundo wa tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi tatu za shina zenye KAK na KA kwa pamoja na uchanganuliwa pia kwa kutumia kanuni ya msingi ya Msambao wa Toni J kuelekea kulia mwa shina la nomino husika.

   c) CJC ni muundo wa tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino ambazo hazina KAK wala KA kabisa na uchanganuliwa kwa kutumia kanuni ya msingi ya Uhamaji wa TJM kwenda silabi ya pili kutoka silabi ya kwanza ya shina la nomino husika.

3. Tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi nne za shina zina muundo wa:

   a) CJJJC ambao uchanganuliwa kwa kutumia kanuni ya msingi ya Msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina la nomino husika.

   b) CJJC kwa nomino za silabi nne ambazo hazina KAK wala KA na uchanganuliwa kwa kutumia kanuni ya msingi ya Uhamaji wa TJM kwenda silabi ya pili kutoka silabi ya kwanza ya shina.

   c) CJCJC kwa nomino za silabi nne za shina zenye TJM mbili na ambazo uchanganuliwa kwa kutumia kanuni ya msingi ya Unakiliji wa TJM katika silabi ya mwisho kasoro moja.

4. Tabia ya ujitokezaji wa toni katika nomino za silabi tano za shina zina muundo wa:

   a) CCJJCJC ambao uchanganuliwa kwa kutumia kanuni ya msingi ya Unakiliji wa TJM katika silabi ya mwisho kasoro moja.

   b) CJJJJC ambao uchanganuliwa kwa kutumia kanuni ya msingi ya Msambao wa toni J kuelekea kulia mwa shina ikifuatiwa na kanuni nyingine za toni.

## MAREJELEO


Batibo, H. M. (2012), Can tone shift be regarded as tone depression in Shisukuma? Katika M. Brenzinger and A.-M. Fehn (Wah.), *Proceedings of the 6th World Congress of*

Goldsmith, J. (1976), "Autosegmental Phonology". Tasnifu ya Uzamivu, MIT. (Imechapishwa).

Goldsmith, J. (1984), Tone and accent in Tonga. Katika. Clements & Goldsmith, 19-51.

Guthrie, M. (1971), *Comparative Bantu,* Juzuu 2, 3, 4. Hants. England: Gregg Press.

Heine, B na Nurse, D. (2000), (Wah.). *African Languages: An Introduction*. Cambridge: CambridgeUniversity Press.

Hyman, L. M. (2003), Basaá (A43). Katika. Nurse & Philippson, 257-282.

Hyman, L. M. (2007), Universals of tone rules: 30 years later. In Tomas Riad & Carlos Gussenhoven (wah.), *Tones and tunes: Studies in word and sentence prosody*, 1-34. Berlin: Mouton de Gruyter.

Hyman, L. M. (2008), Directional asymmetries in the morphology and phonology of words, with special reference to Bantu. *Linguistics* 46. 309-350.

Hyman, L. M. (2010), How to study a tone language, with exemplification from Oku (Grassfields Bantu, Cameroon). *UC Berkeley Phonology Lab Annual Report (2010)*, 179-209.

Hyman, L. M. (2017), Katika. search of prosodic domains in Lusoga. Paper presented at the Workshop on the Effects of Constituency in on Sentence Phonology, University of Massachusetts, Amherst, Julai 30, 2016. Ms. University of California, Berkeley (submitted).

Hyman, L.M na Byarushengo, E.R. (1984), "A Model of Haya Tonology" katika Clements, G. N na J. Goldsmith *Autosegmental Studies in Bantu Tone*, Dordrecht- Holland, Foris Publications, kur. 52-104.

Ismail, J. H. (2011), 'A Tonological Study of Meeto-Makua of Southern Tanzania'. Tasnifu ya uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Ismail, J. H. (2016), *Uchambuzi wa Toni kwa Mkabala wa Kiinitoni na Tonijuu Msingi: Uchunguzi wa Lugha ya ki-Meetto-Makuwa cha Tanzania*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mulika Na. 35.

Kothari, C. R. (2010), *Research Methodology: Methods & Techniques* (Toleo la 6), New Age International Publishers (Ltd), New Delhi.

Marlo, M. R. (2007), 'The Verbal Tonology of Lunyala and Lumarachi: Two Dialects of Luluyia (Bantu, J.30, Kenya)'.Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Michigan (Imechapishwa).

Martinet, A. (2005), *Economie des changements linguistiques*. Paris: Maisonneuve et Larousse.

Mashauri, M. A. (2012), 'Toni katika Nomino za Lugha ya ki-Konongo'. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Massamba, D. P. B. (2011), *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TATAKI.

Massamba, D.P.B. (1984), "Tone in Ci-Ruuri", katika Clements, G.N na J. Goldsmith (Wah) *Autosegmental Studies in Bantu Tone*, Dordrecht-Holland, Foris Publications, uk. 235-254.

Matondo, M. (2003), *Tone and Prosodic Morphology in Kisukuma*. PhD Dissertation. UCLA.

McHugh, B. D. (2006), *The phrasal cycle in Kivunjo Chaga tonology*. Katika. Inkelas & Zec, kur. 217-242.

MLUTA. (2009), *http/www.google.com/lugha/. LOT* (10/4/2018).

Mramba, P. T. (2015), 'Athari za Kirombo katika ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili: vipengele vya Kifonolojia na Kimofolojia'. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Nelson, C. (2013), 'Toni katika Vitenzi vya Kimochi'. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Nurse, D na Phillipson, G. (1977), ''Tones in Old Moshi (Chaga)'', katika *Studies in African Linguistics* 8, kur. 49-80.

Nurse, D. na Philippson, G. (Wah.) (2003), *The Bantu languages*. London: Routledge.

Odden, D. (1989), "Predictable tone systems in Bantu", katika H. van der Hulst na N. Smith (Wah.) *Autosegmental Studies on Pitch Accent Systems*, Dordrecht: Foris. kur. 225–251.

Odden, D. (2005), *Introducing Phonology.* Cambridge: Cambridge University Press.

Polome, S. A. (1971), 'Phonological Survey of the Chaga Dialect of Tanzania'. Tasnifu ya Umahiri, Austin Texas. (Imechapishwa).

Raum, J. (1964), *Versuch einer Grammatik der Dschaggasprache (Moschi-Dialekt)*. U.S.A: The Gregg Press Incorporated.

Van Spaandock, M. (1971), *L'Analyse Morphotonologique dans les Langues Bantoues*. Paris: SELAF.